CHUO CHA BIBLIA

VITABU VYA AYUBU, ZABURI, MHUBIRI NA WIMBO ULIO BORA.

KITABU CHA TANO

VITABU VYA MASHAIRI

Katika mafunzo haya, tutaanza uchambuzi wetu wa vitabu vitano vya mashairi vilivyomo katika Agano la Kale ambavyo ni Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri, na Wimbo Ulio Bora. Vitabu vya Mashairi viko katika mpangilio unaofahamika kama 'Vitabu Vya Hekima' au 'Maandiko,' ili kuvitofautisha na vitabu vya Sheria, Historia, na Manabii katika Agano la Kale.

Vitabu vya Mashairi ni kati baadhi ya vitabu vyenye uvuvio katika maandiko kwa kuwa mashairi ni lugha ya moyoni. Mungu anafahamu umuhimu wa yale ambayo maandiko yanayataja kwa moyo wa watu Wake. Katika sehemu hii ya Biblia, Mungu huzungumza na mioyo ya watu Wake wakati wanapopitia dhiki (Ayubu), wanapoabudu (Zaburi), kukumbana na hali ngumu na kuteswa kila siku katika ndoa, jamii, na katika uzazi, pamoja na fedheha za shughuli za sokoni (Mithali), wakati wanapokumbana na mashaka (Mhubiri), na hatimaye wakati wanapoieleza furaha yao katika ngono kati yake mume na mke (Wimbo Ulio Bora).

Mungu anadhihirisha kuhusika kwake na mioyo yetu wakati anapoviandika vitabu hivi vitano katika maktaba takatifu na yenye uvuvio kwa mashairi, yaani lugha ya moyoni. Tunaposoma vitabu hivi vitano vya mashairi, tunahitajika kuhisi kidole chake Mungu kikigusa moyo wetu–utu wetu wa ndani–kutushawishi kuwa na imani ya kweli ndani mwetu, na kwamba tupate kubadilishwa na ushuhuda wetu pamoja na kutoka ndani hadi nje. Hii ndiyo sababu Mungu ametupatia vitabu hivi vitano vya mashairi.

SURA YA KWANZA

KITABU CHA AYUBU

Kulingana na kitabu cha kwanza kati ya vitabu hivi vitano, maisha ni magumu na yamejaa dhiki kuu ya kuchosha na kushangaza. Watu wake Mungu wamekuwa katika dhiki nyakati zote, nao waumini wengi wamepitia dhiki hata kuuawa kwa ajili ya imani yao baada ya vita vya pili vya dunia mwaka wa 1945, zaidi kuliko katika historia yote ya Kanisa. Kitabu ambacho kinakisiwa kuwa cha zamani sana kuliko vingine ni kile ambacho kinatueleza kuwa uchungu na dhiki ni lazima, lakini

huzuni ni hiari ya mtu binafsi. Kitabu cha Ayubu ni ujumbe wake Mungu kwa mioyo ya watu wake wakati inaumia.

Wengi miongoni mwa wasomi wanakubaliana kwamba kitabu cha Ayubu kiliandikwa nyakati za mababu wa zamani katika jamii ya Kiyahudi. Tunasoma katika kitabu hicho kwamba yeye alipata kuishi miaka mia na arobaini baada ya kuyapata masaibu yake na kwamba *'akafa, mzee sana mwenye kujawa na siku.'* (Ayubu 42:17) Urefu wa maisha yake ni sambamba na umri wao wale tunaowasoma katika kitabu cha Mwanzo.

Mfumo Wa Uandishi Wa Kitabu Cha Ayubu

Swala kuhusu mfumo wa uandishi wa kitabu cha Ayubu linajibiwa wakati tunapotambua sehemu ambayo kitabu hiki kimewekwa katika maktaba hii takatifu ya maandiko. Kitabu hiki ni mmojawapo ya shairi kuu kuwahi kuandikwa. Kitabu hiki cha Ayubu kimeandaliwa kama mchezo wa kuigiza. Hebu fikiria juu ya ujumbe wenye uzito kutoka kwa Mungu kwa mioyo yenye majeraha kama mchezo wenye sehemu tatu. Wakati pazia inapovutwa kwa sehemu ya kwanza, sehemu hii inatupa utangulizi wa hadithi ambayo yamkini ni ya zamani sana katika Biblia.

Sehemu Ya Kwanza

Utangulizi.

Katika onyesho la kwanza ya sehemu ya kwanza, Mungu na Shetani wamo katika mazungumzo kuhusu mtu huyu jina Ayubu. Onyesho la kwanza linatufundisha sisi ukweli mkuu kuhusu vita kati ya wema na uovu. Uovu unadhihirishwa naye Shetani, ambaye ni mwenye shaka kuhusu nia ya Ayubu na wema wake. Mungu akumbana na changa moto lake Shetani kwa jambo ambalo linatajwa na wanathiolojia kama 'ukarimu wa mapenzi yake Mungu' *(permissive will of God).* Mungu huruhusu uovu kutendeka kwenye mipaka ambayo ameiweka kwa kumruhusu Shetani kuchukua kila kitu chake Ayubu, pamoja na wanawe kumi. Shetani amelalamika dhidi ya huyu Ayubu kwamba ni mwenye haki kwa sababu Mungu ameibariki haki yake kwa mali nyingi. Pia alitangaza kwamba kama Mungu angelimruhusu yeye kuchukuwa baraka yake Ayubu, kwa hakika, angelimlaani Mungu.

Kutokana na ukarimu wa mapenzi yake Mungu, na hila mbovu zake huyu Shetani, Ayubu aliwapoteza wanawe wa kiume saba, wa kike watatu, na kondoo elfu saba, ngamia elfu tatu, ng'ombe elfu moja, punda mia tano, na wafanya kazi wengi.

Ingawaje dhiki ilimpata na kumlemea Ayubu, yeye hakumlaani wala kumkufuru Mungu katika shida yake yote. Ayubu alitangaza hivi: *'Mimi nilitoka tumboni mwa mama yangu nili uchi, nami nitarudi tena huko uchi vilevile; Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana na libarikiwe. Katika mambo hayo yote Ayubu hakufanya dhambi, wala hakumwazia Mungu kwa upumbavu.'*(Ayubu 1:21,22). *Confucius* alisema, *'Tulikuja katika ulimwengu huu hali mikono yetu imekunjwa tukivitaka vitu vyote bali tutautoka ulimwengu huu mikono yetu imekunjuliwa. Tukiwa hatuna cho chote kile.'* Ayubu anatuambia mikono yake ilikuwa imekunjuliwa alipozaliwa. Mali yake yote iliwekwa katika mikono yake na Mungu,-naye hakuwahi kuikunja. Mali ile ilikuwa ni yake Mungu wakati alipoiweka katika mikono yake. Ilikuwa yake Mungu na angeichukua wakati wo wote apendezwaye.

Ayubu alifaulu mtihani wake wa kwanza vyema sana! Tunahitajika kutambua kwamba Ayubu hakuwa sawa aliposema kwamba Bwana ndiye aliyewachukua wanawe pamoja na mali yake yote. Tunafahamu hivyo kwa sababu tunauona utangulizi wa yale yaliyotendeka kwamba alikuwa ni Shetani aliyechukua mali yote ya Ayubu.

Hebu tambua jinsi Ayubu alivyoipoteza mali yake. Aliwapoteza wanawe kumi kwa tukio la upepo wenye nguvu uliovuma kutoka jangwani na kuipiga nyumba ya mwanawe wa kwanza wa Ayubu. Akawapoteza kondoo wake na wachungaji kutokana na 'moto wa Mungu ulioanguka kutoka mbinguni', ambao labda ulitokana na umeme na radi. Bima hulielezea tukio kama hili kuwa 'Tendo la Mungu.' Sisi kwa hakika tunafahamu kwamba haya hayakuwa ni matukio kutoka kwa Mungu, bali kutoka kwake Shetani; kufuatia ruhusa aliyopewa na Mungu. Lakini Ayubu hakufahamu hivyo.

Shetani pamoja na Mungu wamo kwenye mazungumzo mengine kumjadili Ayubu. Mungu anatukuza kwa mara nyingine kuwa ndiye mfano bora wa mtu mwenye haki. Kwa mara nyingine, Shetani naye awasilisha malalamishi kuhusu nia au kusudi lake Ayubu kuwa haki. Yeye anatangaza kwamba hakika huyu Ayubu atamlaani Mungu ikiwa atamruhusu Shetani kumdhuru. Mungu tena anampa ruhusa Shetani kumdhuru Ayubu mwenyewe–kwa sharti moja tu. Asiuchukuwe uhai wake Ayubu. Unaweza kusema kwamba Mungu alimruhusu Shetani kumtesa kwa sababu hayo ndiyo maana ya kumtesa–kumdhuru kwa uchungu mwingi bila kuchukua maisha yake. Ayubu anapigwa na

majipu mabaya tangu wayo wa mguu hata utosi wa kichwa. Wasomi hufikiri kuwa ulikuwa ugonjwa wa kuvimba miguu- matende au Jethamu, namna ya saratani ambayo hubadilisha rangi ya mwili kuwa kama ngovi ya ndovu pamoja na vidonda vya ukoma vyenye usaa. Ayubu aliteseka jinsi mwanadamu anavyoweza bila kuona mauti.

Ayubu hakumbani na hatua ya pili ya majaribu vyema. Mkewe anamshauri amlaani Mungu ili apate kufa. Lakini yeye anajibu: *'Wewe wanena kama mmoja wa hao wanawake wapumbavu anenavyo. Je! Tupate mema mkononi mwa Mungu, nasi tusipate na mabaya?* (Ayubu 2:10). Hakika, Ayubu alikuwa akiuliza, *'Mtu mwenye haki atakikana kutarajia Mungu kuweka kitu gani katika mikono yake kwa kuwa yeye ni mwenye haki?'*

Sehemu kubwa katika kitabu cha Ayubu imefanywa utangulizi kwa swali hili ambalo Ayubu alimwuliza mkewe. Kabla ya pazia kufungwa baada ya sehemu ya kwanza, Ayubu atembelewa na marafiki wa zamani wenye hekima. (2:11). Wao wanakutana pamoja ili kumfariji. Sawa na Ayubu, wao wana umri wa kukomaa na walitambulikana kama wenye hekima na watu wa dini. Katika siku ya leo tunawaita wanathiolojia. Wao pia wanashangazwa na hali ya afya yake Ayubu hivi kwamba wanakaa kimya pamoja naye kwa siku saba. (Baadaye, Ayubu atawaeleza kwamba juma hilo moja la kimya lilikuwa ndilo tendo jema zaidi katika faraja yao.) Pazia linashushwa baada ya sehemu ya kwanza huku Ayubu akiwa ameketi na kuzingirwa kwa kimya na marafiki wake.

Sehemu Ya Pili

Kushirikiana

Wakati pazia inapofunguliwa kwa sehemu ya pili, tunajulishwa kwa marafiki wake Ayubu watatu, Elifazi, Bildadi, na Sofari. Huku wakiwa wameketi chini naye Ayubu kwa kimya cha huzuni kwa siku saba za kwanza, wao walikuwa ni mfano bora wa faraja kwa kuwa walimfariji Ayubu kwa uwepo wao. Wakati watu wanapopitia katika dhiki, uwepo wa marafiki zao ni wa muhimu sana kuliko maneno.

Hata hivyo, marafiki wake Ayubu walifanyika kuwa wafariji wasio na faraja wakati walipoanza kuzungumza kuhusu dhiki yake. Ayubu afungua sehemu hii ambayo tunalitaja kama, 'Kushirikiana' katika mazungumzo ambayo yeye ailaani siku yake. Yeye hamlaani Mungu jinsi Shetani alivyokuwa akitarajia. Mfumo wa sehemu hii ndefu sana katika kitabu hiki ni kwamba, baada ya Ayubu

kuyafungua yale mazungumzo, mmoja wa hao marafiki wake atayatoa mazungumzo ambayo yatafuatiwa na upinzani kutoka kwake Ayubu. Wao wazunguka kwa mviringiko ule wakilitenda jambo hili kwa mara tatu.

Elifazi alidai kwamba yeye alikuwa amelipokea neno moja kwa moja kutoka kwake Mungu, kwa njia ya kibinafsi ya kiroho ambayo ulimwonyesha mwanadamu kuwa chini ya rehema za haki ya Mungu. Kupitia ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwake Mungu, aliweza kumwambia Ayubu kwa ukakamavu kwamba dhiki yake ilitokana na dhambi iliyokuwa katika maisha yake. (Ayubu 4:12-21). Bildadi aliamua kwamba Ayubu alikuwa akiteseka na kwamba wanawe walifariki kwa sababu ya dhambi zao. (8:1-7). Pia alidai kwamba Ayubu alikuwa mwenye dhambi. Sofari alikuwa mwenye elimu ya kutoamini mambo ya kawaida–zaidi ni kutegemea maarifa yatokayo na ujuzi, na kuilinganisha na ile elimu yao yaani *(Agnostics.* Yeye alidai kwamba mwanadamu hawezi kufahamu kwa nini anateseka, bali akasema kwamba kulifikiria jambo hilo ni busara na jambo la kufanywa. (11:7-12). Yeye aungana nao na kukubaliana na marafiki zake kwamba chanzo cha masaibu ya Ayubu ni dhambi iliyo katika maisha yake. Hawa 'wafariji' watatu wanamhimiza Ayubu kuziungama dhambi zake.

Kumalizia haya mazungumzo, Ayubu pamoja na marafiki wake walikumbana na lile swala ambalo Ayubu alimwuliza mkewe*, 'Ni jambo gani ambalo mtu wa haki hastahili kutarajia kutoka kwake Mungu kuliweka katika mikono yake kwa kuwa yeye ni haki?*' Wote walikubaliana kwamba Mungu huyaweka mambo mema katika mikono ya mtu mwema na yaliyo maovu aliye muovu. Tatizo lao lilikuwa kwamba Ayubu alionekana kana kwamba yeye ni mtu mwenye haki naye Mungu alikuwa akiviweka vitu viovu katika mikono yake. Sitofahamu kati yao ilikuwa kuu na yenye joto kali huku wakijaribu kulitatua tatizo lile.

Kote katika mazungumzo haya kati ya Ayubu na marafiki zake, wao walikubaliana kwamba Ayubu alikuwa muovu. Kwa sababu yeye alionekana kana kwamba ni mwenye haki, wote walikubaliana kwamba ni lazima awe alikuwa na dhambi ya siri katika maisha yake. Mmoja wao alimwita Ayubu kuwa ni buu na kumwambia kwamba Mungu alikuwa akimwadhibu kidogo kuliko alivyostahili. Mwingine aliamini kwamba ilikuwa ni dhambi katika maisha ya wanawe Ayubu ambayo ilikuwa imemfanya Mungu kuyachukua maisha yao na kumwadhibu Ayubu kwa dhiki hiyo. Wote walimhimiza Ayubu kuitubu dhambi pamoja na kukiri. Na hivyo, unaweza kuona kwa hakika kwamba maongezi yao hayakumfariji huyu Ayubu.

Katika mazungumzo yake, Ayubu alitilia mkazo kwamba yeye alikuwa mwenye haki. Yeye alisisitiza kwamba alikuwa mwenye haki hivi kwamba akatilia shauku haki yake Mungu kumpa dhiki katika mikono yake. Mazungumzo haya yanamalizika wakati wafariji wake Ayubu wanapokubaliana kwamba wao hawawezi kumshawishi kwamba ni mwenye dhambi.

Ingawaje marafiki zake Ayubu walikuwa wasomi na watu wa kiroho, Mungu baadaye aliwaambia hivi, *'Nyinyi mlikuwa mmekosea kwa yale mliyoyasema kunihusu mimi, na pia mlikosea kuhusu yale mliyoyasema kumhusu mtumishi wangu Ayubu.'*(42:7-9).

Baada ya Ayubu kuzungumza na Mungu kwa njia ya upepo mali wa kisulisuli, tunamsikia akisisitiza wakati wote katika maongezi yake na marafiki kwamba yeye ni mwenye haki, na kwamba yeye si muovu. (40:4). Unapozidi kusoma maongezi ya rafiki zake Ayubu, kumbuka kwamba mwishoni mwa kitabu hiki, Mungu anawaambia kwamba yale yote waliyoyasema kumhusu Ayubu yalikuwa sio kweli na kwamba yale waliyoyanena kumhusu Yeye pia yalikuwa ni makosa. Unaposoma maongezi ya Ayubu yenye utetezi kuhusu haki yake ya kibinafsi, tambua kwamba hapo mwisho wa kitabu hicho, Ayubu anamwona Mungu na kujidharau mwenyewe hata kutubu katika majivu na vumbi. Jiulize mwenyewe 'Mbona Ayubu alijidharau mwenyewe na je, alitubu kwa nini?'

Tunasoma kwamba marafiki wake Ayubu walikubaliana kwamba wao hawawezi kumshawishi kuwa dhambi ndiyo chanzo cha dhiki yake, na tuseme kwamba maneno yake Ayubu yamefikia mwisho, pazia linafungwa kudhihirisha mwisho wa sehemu ya pili.

Sehemu Ya Tatu

Suluhisho.

Pazia linapofunguliwa katika sehemu ya tatu, Ayubu, na marafiki zake bado wangali wameketi kwa mviringo lakini yupo mtu mwingine pamoja nao. Jina lake ni Elihu, naye ni kijana kumliko Ayubu na marafiki zake. Huyu kijana anazungumza na kueleza kwamba alikuwa amejizuia kusema kwa kuwa yeye ni kijana ilhali wao ni wazee sana kwa hivyo alijiziuia, asithubutu kuwaonyesha aonavyo. Hata hivyo, kwa sababu mbili, yeye aliamua kuzungumza. Kwanza kabisa, anatambua kwamba hekima hutoka kwa Roho Mtakatifu na umri wake mtu haujalishi. Sababu ya pili

kuzungumza ni kwamba alitambua kwamba wao hawangelitatua tatizo lao kwa kuwa walikuwa wakiuliza maswali yasiofaa.

Suluhisho kwa tatizo la dhiki yake linapatikana katika maongezi yake Elihu na jibu lake Ayubu kwa mjadala ule. Kwa kina cha mjadala wake, Elihu alimwambia Ayubu kutazama juu na kuona nia yake Mungu kuhusu dhiki yake. Kulingana na kijana huyu mwenye uvuvio, swali ambalo Ayubu aliuliza mkewe lilikuwa bovu kwa kuwa liliuweka mkono wake Ayubu katikati ya dhiki yake. Elihu alibadilisha swali hilo na lingine jema: *"Je! Wewe wadhani kwamba haya ni haki yako, au je! Wasema, Haki yangu ni zaidi kuliko ya Mungu, maana wasema, Kutakuwa na faida gani kwako wewe? Tena, nitapata faida gani, kuliko nikifanya dhambi? Mimi nitakujibu, Na wenzio pamoja nawe. Ziangalie mbingu ukaone; na mawingu yaangalie, yaliyo juu kuliko wewe. Ikiwa umefanya dhambi, umefanya nini juu yake? Yakiwa makosa yako yameongezeka, wamfanyia nini yeye? Ikiwa u mwenye haki, wampa kitu gani? Au yeye hupokea nini mkononi mwako?* (Ayubu 35:2-7).

Kuunyosha mkono wako katikati mwa dhiki yako na kuuliza, '*Ni kipi ambacho Mungu atakiweka katika mkono wangu?'* ni swali ambalo si sawa kwa mtazamo huu na katika uhusiano wetu naye Mungu. Kusudi lake kuu mwanadamu ni kumtukuza Mungu. Hili linamaanisha kwamba tuweke mkono wa Mungu ulionyoshwa kila mara katikati mwa dhiki yetu, na katika maisha yetu huku tukiuliza hivi, *'Ni kitu kipi ambacho Mungu atapokea mkononi mwangu?'*

Kumbuka kwamba shutuma zake yake Shetani dhidi ya Ayubu ni zile ambazo twazitaja kama muumini ambaye hutengemea haja zake. Kama wale waliokuwa wakimfuata Yesu kwa sababu ya mkate na samaki, Ayubu alikuwa amenyosha mkono wazi huku akiishi maisha ya haki. Hapo awali, niliuliza swali hili, 'Ni kwa sababu gani Ayubu alijidharau alipomwona Mungu?' na, ni 'kwa sababu gani Ayubu alitubu baada ya kumwona Mungu?' Naamini kwamba Ayubu alitambua, kupitia mazungumzo yake pamoja na Elihu kwamba yeye alikuwa ameunyosha mkono wake wazi katika uhusiano wake na Mungu. Yeye hakufahamu kwamba ilikuwa hivyo hadi wakati Mungu alipotuma dhiki kudhihirisha hayo kwake. Ni wakati alipoona kwamba alikuwa akimtumia Mungu alipojidharau mwenyewe na kutubu katika majivu na mavumbi.

Ingawa kulikuwa na sitofahamu kati ya Ayubu na wafariji wake kupitia mazungumzo yao, yeye hakutofautiana na huyu kijana. Alitenda yale kijana huyo aliyomshawishi kufanya. Yeye atazama juu na punde tu akamwona Mungu ndani ya upepo makili wa kisulisuli.

Yeye na Mungu walifanya maongezi kwa muda na baadaye akatangaza hivi: *'Tazama mimi ni muovu;….nalifunika kinywa changu kwa mkono wangu….sitaendelea mbele.'* Baada ya maongezi yake pamoja na Mungu, Ayubu asema: *'Nilikuwa nimesikia habari zako, kwa kusikia kwa masikio; Bali sasa jicho langu linakuona. Kwa sababu hiyo najichukia nafsi yangu, na kutubu katika mavumbi na majivu.'* (Ayubu 42:5-6).

Baada ya toba yake Ayubu, Mungu anawakemea marafiki zake Ayubu. Wakati jambo hilo linatendeka, Ayubu anawaombea marafiki zake. Pia wakati Ayubu anapowaombea marafiki zake, Mungu anaifanya mara mbili mali yake. Pazia linaposhushwa chini kwa sehemu ya tatu, Mungu tayari ameifanya mali yake yote Ayubu kuwa mara mbili na wana wengine saba pamoja na binti watatu.

Mambo Ya Kutimizwa Kibinafsi

Kitabu hiki cha mwanzo katika vitabu vitano vya mashairi ni Neno lenye uvuvio wake Mungu kwa watu wenye mioyo inayoumia. Hivyo basi, hadithi hii maarufu ya kale kuhusu maumivu inaweza kutazamwa kama mfano dhahiri wa mmojawapo ya Heri zake Yesu katika Mahubiri yake juu ya Mlima: *'Heri wenye huzuni; kwa maana hao watafarijika.'* (Mathayo 5:4). Mara nyingi funzo katika Agano Jipya hufafanuliwa na kufanywa kuwa maelezo katika Agano la Kale. Katika Agano Jipya, Yesu ametupa funzo hili kuu kwa sentensi moja, lakini katika kitabu cha Ayubu, ukweli ule watumiwa katika tukio lenye kudhihirika na kufundisha hatua tatu ambazo tunaweza kuzichukua ili kupokea faraja na baraka ambayo Kristo aliwaahidi wale wenye huzuni. Hatua hizo tatu ni hizi:

Hatua Ya Kwanza: Achilia huzuni yako ikupeleke mahali ambapo yamkini kwa mara ya kwanza katika maisha yako, unaweza kuuliza maswali mema. Tazama jinsi Ayubu alivyouwa mfano bora kwetu. Unapozidi kusoma kitabu hiki, taama jinsi Ayubu alivyosukumwa na dhiki yake ili kuuliza maswali kama: *'naam mwanadamu hutoa roho, naye yupo wapi? Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena? Na kama mwanadamu akifa, je! Yeye ataishi kwa mara nyingine?'* (14:10,14) Haya ni baadhi ya maswali ambayo sisi twahitajika kuyauliza wakati tunapopitia katika dhiki na huzuni.

Hatua Ya Pili: Achilia huzuni yako ikupeleke mahali utakaposikiliza majibu yake Mungu kwa maswali sahihi. Ayubu aliuliza. *'Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena?'* Mungu alijibu swali hilo wakati alipomrudishia Ayubu mali yake mara mbili. Fahamu kwamba Mungu alifanya mara mbili mifugo yake

Ayubu, lakini hakuwarudifisha wanawe mara mbili, ila tu alimrudishia wana wa kiume saba na binti zake watatu baada ya kufanya mara mbili mali nyingine yote yake Ayubu.

Maelezo ni kwamba wakati mifugo wake walipofariki, wao walikuwa wafu, lakini wakati wanawe pamoja na binti zake walipofariki, wao walikuwa bado hai katika hali ya uzima. Ili kuwafanya wanawe kuwa mara mbili, ilimbidi Mungu kumwongezea Ayubu wana wengine saba pamoja na binti watatu wa ziada. Kwa hali hiyo ya kuishi milele, Ayubu alipata kuwa na wana wa kiume kumi na wanne pamoja na binti wengine sita. Hii ni njia mojawapo ambayo Mungu alimjibu Ayubu swali lile, *'Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena?'*

Katika maandiko, utapata majibu mengi sana kwa swali hilo, jinsi Mungu alivyomjibu Ayubu. Zaburi sura ya ishrini na tatu, na katika Agano Jipya mahali Yesu anatueleza kwamba yeye ndiye huo ufufuo na uzima, na kwamba ye yote yule amwaminiye hajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kumwamini hatakufa kabisa hata milele. (Yohana 11:25, 26). Wakati unaposoma maandiko, utapata baadhi ya majibu mengi ya kuvutia kutoka kwa Mungu kupitia maswali mazuri. Kwa njia ya maombi, yatafute na kusikiliza kwa makini sana huku Mungu akikuongoza kwenye majibu hayo ya kuvutia kwa maswali mema yaliyo katika Neno lake Takatifu.

Hatua Ya Tatu: Achilia huzuni yako ikupeleke mahali utakapoamini majibu yake Mungu kwa maswali yaliyo mema. Unapouliza maswali mema, na kusikiliza majibu yake Mungu kwa maswali yale, na kuyaamini, utagundua baraka na faraja ambayo Yesu aliwaahidi walio na huzuni. Biblia inataja baraka na faraja hizo kama 'Wokovu.'

SURA YA PILI

Sababu Thelathini Kwa Nini Watu Wake Mungu Hupita Kwenye Dhiki Au Huteseka.

Kwa maelfu ya miaka, watu wake Mungu wamekuwa wakiuliza, 'Mbona watu walio haki huteseka?' Kitabu cha Ayubu ni ufafanuzi bora zaidi na kina ufasaha mkuu kwa kujibu swali hilo. Lakini, kitabu hicho sio cha pekee ambapo unaweza kulipata jibu hilo katika Biblia. Kutoka Mwanzo

hadi Ufunuo, utagundua kwamba dhiki ya watu imetajwa katika Neno lake Mungu. Katika sura hii, nitagusia kwa ufupi maelezo thelathini katika Biblia kuhusu dhiki.

1. Dhiki hutufundisha kwamba Mungu mwenyewe ndiye kina cha faraja zote. Wazo moja lilimpa Paulo faraja alipokuwa akikabiliana na majaribu magumu huko Arabuni: *'Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote.'* (2 Wakorintho 1:3). Dhiki ilimfanya Paulo kuvumbua kwamba Mungu alikuwa pamoja naye na angeliweza kumfariji. Yeye anatupa changa moto tuvumbue hayo wakati tunapokuwa wenye dhiki.

2. Dhiki hufunza, hutuvisha silaha, hututayarisha kuwafariji wengine: Paulo alizidi katika wazo hilo aliloanza katika fungu ambalo limetajwa hapo kwa kuandika hivi: *'Atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo tunazofarijiwa na Mungu'* (2 Wakorintho 1:4). Minjilisti ni maskini mwombaji mmoja akimweleza maskini mwombaji mwingine mahali mkate upo. Mhudumu aliyefaulu katika faraja ni yule aliye na moyo wenye maumivu anayemweleza mwenzake aliye katika hali sawa na hilo mahali faraja ipo. Tunapovumbua faraja ambayo inapatikana kwa Mungu mwenyewe, huwa tunafaulu kama wahudumu wa faraja. Ni wale tu ambao wana ushuhuda wa dhiki ambayo iliwapeleka kuvumbua faraja yake Mungu ambayo unaweza kuwaambia wengine walio na mioyo yenye maumivu pale faraja ipo.

3. Dhiki hutupeleka kuitafuta hekima yake Mungu. Kulingana na Yakobo, wakati dhiki inapotuweka kwa hakika katika hali ambayo hatufahamu la kufanya, tunahitajika kumwomba Mungu hekima ambayo tunaikosa. *'Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa'* (Yakobo 1:5). Yakobo anatuhakikishia kwamba Mungu atatupa hekima tunayohitaji.

4. Dhiki hutuongoza kukomaa kiroho: Yakobo alifundisha kwamba dhiki hutufanya kuwa *'Wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno'* (Yakobo 1:4). Jaribio la imani hutuongoza katika tumaini ya imani. Tumaini ya imani hutuongoza katika ushindi wa imani, au 'taji ya uzima' (12).

5. Dhiki hutufungulia njia kwa neema yake Mungu: Wakati Mungu anapotupatia hekima kwa kuwa hatufahamu la kutenda, pia tunahitaji neema Yake ili kwamba tukatekeleze hekima hiyo Yake. Paulo aliandika: *'Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema.'* (2 Wakorintho 9:8). Neema yote, ninyi nyote, wakati wote, kujitosheleza kote, vitu vyote, kuongezeka, kazi nzuri. Na ndio sababu Paulo anatuambia kwamba tufurahi katika dhiki ambayo hutupeleka kuvumbua nyumba ya hazina ya hekima na neema.

6. Dhiki huzalisha tabia ya kiroho: Dhiki huzalisha dhamana ya tabia ndani mwetu ambayo haitoki hata mambo yanapofanyika kuwa magumu*: 'Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitayaharishi.'* (Warumi 5:3-5a). Maneno haya kama subira na tabia yenye kudhihirika yanaeleza kile ambacho tunaweza kuita, 'Uwezo wa Kudumu.' Hii ni tabia ambayo huning'inia pale na hubaki imening'inia bila kujali jinsi mambo yalivyo magumu. Hivi ndivyo chungwa hufanyika kuwa chungwa. Hilo huning'inia huku likishikamana na mti hadi wakati ambapo litafanyika kuwa ni chungwa. Dhiki inaweza kuendeleza hali hii ya tabia ya kiroho.

7. Tunapopitia katika dhiki nyakati za ujana wetu, huwa tunapokea uwezo kwa wakati ule wa utu uzima wa wetu: Maombolezo 3:27 hufundisha, 'Ni vema mwanadamu aichukue nira wakati wa ujana wake.' Wakati vijana wa kike na kiume wanapojaribiwa, wao huendeleza nguvu na uthabiti wao kwa kuwa watahitaji kuvumilia majaribu wakati watakapokuwa wazima.

8. Dhiki huwafunza wahudumu wa Injili: Paulo aliandika kwamba dhiki ni njia ya kututhibitisha kuwa wahudumu wake Mungu: *'Bali katika kila neno tujipatie sifa njema, kama watumishi wa Mungu; katika saburi nyingi, katika dhiki, katika misiba, katika shida.'* (2 Wakorintho 6:4). Mungu hupenda sisi tuitikie *'katika kuwa safi, katika elimu, katika uvumilivu, katika utu wema',* na tuzipate rasilmali za kutuwezesha kuitika *'katika Roho Mtakatifu, katika upendo usio unafiki, katika neno la kweli, katika nguvu ya Mungu.'* (6, 7a). Dhiki ni uwezo ambao Mungu hutumia ili kuthibitisha 'Seminari' ambayo Yeye huwatayarisha wahudumu wa Injili.

9. Dhiki huzalisha ‘Jiwe la vipimo vya miujiza’ katika safari yetu ya imani: Wakati Daudi alipoomba kwa ukombozi nyakati za dhiki yake kuu (Zaburi 3:1-6), Yeye aliomba kwa imani iliyotambulikana kwa ujasiri kwa kuwa alikuwa ameuthibitisha uaminifu wake Mungu nyakati za pingamizi katika maisha yake hapo awali. Kila wakati tunapothibitisha kwamba Mungu yupo hata nyakati za pingamizi kuu, huwa tunaongezea ‘alama za miujiza’ ambazo hutuongeza nguvu na kututia moyo katika imani zetu kwa wakati huu na wakati ujao katika pingamizi tutakazokumbana nazo katika maisha yetu.

10. Dhiki huyanyosha mapito kwa wokovu wake Mungu: Isaya alihubiri kwamba maisha yake Masihi yangalikuwa kama njia kuu ambayo Mungu angeuleta wokovu kupitia hadi ulimwengu huu*: ‘Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa’* (Isaya 40:4). Maisha yake Yesu yalikuwa njia kuu ambayo Mungu na wokovu alisafiri hadi ulimwengu huu. Kuwa kama Kristo kunamaanisha kwamba tunahitajika kuwa kama njia kuu ambayo Mungu huleta wokovu katika ulimwengu huu kutupitia. Mungu anaweza kuwaletea wokovu watu wengine kupitia maisha yetu wakati milima yetu ya kiburi inaposhushwa, na bonde zetu kujazwa, dhambi zetu zilizopopotoka zinyoshwe, na mahali palipoparuza pasawazishwe.

11. Dhiki ni dhihirisho la uweza wake Mungu: Paulo alipoomba kwamba Mungu apate kumwondolea mwiba uliokuwepo mwilini mwake, Mungu alimwambia hivi, *‘Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu’* (2 Wakorintho 12:9). Udhaifu wetu ni dhihirisho la nguvu na uweza wake Mungu. Hii ni mmojawapo ya maelezo kuhusu uchovu mwingi unaotokana na dhiki nyingi. Udhaifu wetu unaweza kuwa ni dhihirisho ya uweza wake.

12. Upungufu wetu unaweza kuonyesha kutosheleza kwake Mungu: Dhiki kwa wakati mwingi hutufanya kuwa na upungufu. Paulo alikuwa amedhoofika sana kwa ajili ya mwiba uliokuwa mwilini mwake. (2 Wakorintho 12:10). Ilhali wakati tunapokuwa wanyonge, Mungu naye huwa mwenye nguvu. Wakati sisi hatuwezi, Yeye anaweza. Mungu anaweza kutumia dhiki kutufahamisha wakati uwezo wetu unapofika ukingoni na wakati uwezo wake unapochukua usukani.

13. Dhiki ni fursa ya kutufundisha juu ya kunyenyekea: Paulo aliandika kwamba mwiba uliokuwa katika mwili wake ulitumiwa *'makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi',* kwa wingi wa mafunuo hayo alipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani *'ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi.'* (2 Wakorintho 12:7). Kwa wakati mwingine yeye hutumia dhiki kutufanya kuwa wanyenyekevu kwa kuwa tunaweza kujaribiwa kuwasikiliza wenye kuvutiwa nasi wakati Mungu anapotutumia, na kumnyang'anya utukufu ambao wastahili Yeye.

14. Ushuhuda utokao katika dhiki wakati mwingi hutuongoza katika ushuhuda wa furaha: Katika Zaburi sura ya 126, tunasoma hivi: *'Wapandao kwa machozi Watavuna kwa kelele za furaha'* (5) Machozi ambayo sisi humwaga nyakati za dhiki huwa ni 'mbegu' ambazo wakati ujao zitazaa tunda la furaha. Ingawa dhiki hudumu kwa muda tu, mara kwa mara huzaa furaha wakati wa mavuno. Wakati mwingine ni lazima tungojee kwa hali ya kimilele ili tupate ujuzi ule wa kuyapiga makelele ya furaha.

15. Dhiki wakati mwingine ni kama 'jambo la kuchuja' ambalo huonekana kama kurudishwa nyuma: Yesu alifundisha kwamba tu matawi yake naye ndiye mzabibu. Ili kuzaa matunda, ni lazima wakati wote tudumu katika uhusiano pamoja naye Kristo ambaye ndiye mzabibu wetu; jinsi tawi lilivyo kwa mzabibu. Ili kuwa na uzao mwingi, ni lazima tuvumilie uchungu wa taratibu ya kufyeka au kupogoa matawi, lakini kupogoa huongeza mazao na furaha ya maisha katika Kristo (Yohana 15:2-11).

16. Dhiki humdhihirisha Kristo Kwa Ulimwengu: Paulo aliandika kwamba wakati tunapokuwa katika dhiki, huwa tu vyombo vya udongo ambavyo ni lazima tuivumilie dhiki ili tupate kudhihirisha adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu katika Kristo, ambaye ni kama nuru kuu wenye kuangaza ulimwenguni kupitia nyufa zilimo kwenye chombo hicho (2 Wakorintho 4:7-10). Tukiwa katika dhiki, huwa *'twadhikika, bali hatusongwi'*, huku tukidhihirisha uzima wa Yesu katika miili yetu.

17. Dhiki inaweza kuzindua kukua kwa utu wetu wa ndani: Utu wa nje ni wa muda tu, lakini utu wa ndani ni wa milele. '*Wakati utu wa nje anapozidi kuchakaa, utu wa ndani anaweza kufanywa upya siku baada ya siku na kutayarishwa kwa utukufu wa milele'* (2 Wakorintho 4:16) *maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo kidogo tu, lakini yatufanyia utukufu*

wa milele uzidio kuwa mwingi sana.' Hii ni dhana ya kushangaza mno ya kushiriki pamoja na wale ambao wamo katika dhiki itokayo katika uovu ambao unawaongoza uzima wa milele.

18. Dhiki inaweza kutufunza dhamana za milele: Tunaelezwa kwamba katika siku za mwisho, ulimwengu utatetemeshwa hadi vile visivyowezwa kutetemeshwa vikae (Waebrania 12:25-29). Kwa kuwa maisha yetu ni ya kitambo tu, nazo dhamana zetu wakati mwingi huwa zimeshikiliwa na mambo ya kitambo kidogo tu ya ulimwengu huu, nao wakati mwingine Mungu hutumia dhiki ili kuyainua macho yetu kutoka kwa mambo hayo ya kitambo kidogo na kuweka mtazamo wetu kwa dhamana za uzima wa milele.

19. Dhiki hutusafisha: *'Mungu wetu ni Moto ulao.'*(Waebrania 12:29). Wakati mwingine yeye hutumia dhiki kuteketeza cho chote kilio katika maisha yetu ambacho ni kinyume na asili takatifu yake Mungu. Taratibu hii ya utakaso ambayo hututayarisha kwa uzima wa milele, inaweza kutujia kwa hali ya dhiki.

20. Dhiki wakati mwingine ni mavuno ya uchaguzi au hiari mbovu: Sisi huvuna yale tuliyopanda. Tukipanda uharibifu, hakika tutavuna uharibifu. Nia iliyopotoka huongoza katika maisha yaliyopotoka. Kwa wakati mwingine, tunapokuwa katika dhiki, huwa tunavuna 'karamu ya matokeo' kwa kuwa sisi tumepanda mbegu mbovu katika shamba la maisha yetu. (Wagalatia 6:7,8).

21. Dhiki huthibitisha utu wetu kama wana wake Mungu: Mungu kwa uaminifu huwaadhibu wale ambao kwa hakika ni wana wake (Waebrania 12:4-11; Yohana 1:12,13). Yeye huchukua wajibu wa wana wake ambao hautumii kwa wale ambao hawamwiti Baba au Bwana. Kwa kuwa yeye ni Baba yetu, nasi tu wanawe, yeye hutuadhibu tunapotenda dhambi.

22. Dhiki humaanisha kuwa Kristo anatamani ushirika wetu: Kristo aliyefufuka, aishiye yupo mlangoni mwa roho zetu akibisha kwa wale ambao ni vuguvugu- wale wasio moto wala baridi katika kujitolea kwao kwake. Kubisha huku kunawakilisha adhabu na maonyo yake kwa kuwa sisi tunamtaja kama Mwokozi lakini hatumwiti Bwana (Ufunuo 3:19,20). Yeye anapenda kuingia mahali penye dhamana kuu, pamoja na kushirikiana katika maisha yetu. Kubisha huku kwa Kristo kunaweza kutokea kwa njia ya dhiki.

23. **‘Zizi la Nguruwe’ huwafanya wapotevu kurudi:** Jinsi mwana mpotevo *‘alipozingatia moyoni’* wakati alipokuwa katika dhiki kwenye zizi la nguruwe (Luka 15:17), vivyo hivyo kuwa na dhiki katika ‘zizi la nguruwe’ la ulimwengu huu kunaweza kutufanya kuzingatia, na kutuongoza katika toba na kutufanya kumrudia Mungu kwa dhati; na kuwa na ushirika kwa dhamana zake Baba.

24. **Dhiki na adhabu hutufanya kushiriki katika utakatifu wake Mungu:** Wakati Baba yetu wa mbinguni anapotuadhibu katika pendo, huwa tunajifunza kwamba: *‘Yeye huturudi sisi kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake.’* Mungu ni mtakatifu, naye anataka sisi tuwe watakatifu. Mara kwa mara yeye hutumia dhiki kutusaidia kufahamu umuhimu wa utakatifu katika tabia Yake na yetu (Waebrania 12:10).

25. **Sisi hupata dhiki kwa kuwa ulimwengu unamchukia Kristo pamoja na wafuasi wake:** Mtume Paulo aliandika hivi *‘. . .wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa’* (2 Timotheo 3:12).

26. **Dhiki huitakasa imani yetu:** Petro aliandika kwamba: *‘…ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbali mbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo’* (1 Petro 1:6-7). Jinsi vile dhahabu husafishwa kwa moto, imani yetu ambayo ni ya thamani kuu kuliko dhahabu, husafishwa kwa ‘moto’ wa dhiki yetu.

27. **Tunakubwa na dhiki, huwa tunaufuata mfano wake Mwokozi wetu:** Petro aliandika kwamba tumeitwa ili ‘tufuate nyayo zake.’ (1 Petro 2:21). Yeye aliteseka kwa uchungu wa msalaba kwa ajili ya wokovu wetu. Alisema wazi wazi kwamba tunahitajika kuubeba msalaba wetu na kufuata mfano wake (Luka 9:23-25; 14:25-35). Sisi twazifuata nyayo zake wakati tunapovumilia dhiki kwa ajili yake.

28. **Mara kwa mara dhiki wakati hufungua mlango kwa ufalme wake Mungu:** Wakati Paulo na Barnaba walipokuwa wamedhihakiwa katika safari zao za umishionari, waliwatia moyo waumini wengine *‘wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani,*

na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi.' (Matendo 14:22). Ingawa hatupaswi kuwa katika dhiki ili kuingia katika ufalme, wengi wameletwa katika imani kupitia lango la dhiki kuu.

29. Ni lazima sote tuingia katika uzima wa milele kupitia kifo na ufufuo wetu: Yesu alimwambia yule mwanamke Martha kwamba shida kuu mbili ambazo hazijasuluhishwa za magonjwa na mauti zinaweza kuwa lango ambalo hutuongoza kuishi milele (Yohana 11:20-32). Tunaweza kubadilisha hizo shida mbili kuwa tikiti zetu za kwenda mbinguni kwa kuamini kwamba Yesu ndiye suluhisho la kipekee kwa shida hizo. Mungu hawezi kuondoa magonjwa na mauti, lakini hili linaweza kutupokonya kwa njia ya kipekee ya kutoka katika ulimwenguni huu. Haya ni maelezo mengine ya kibiblia ambayo yanakutupa sababu ya kupitia katika dhiki.

30. Falsafa ya kibibilia kuhusu mauti: Ili kuthibitisha mamlaka ya uongozi wake, mchungaji wakati mwingi ni lazima awapige kwa fimbo kondoo kwenye vichwa vyao ile wapate kujilaza chini. Kulingana na Daudi, Mungu hufanyika kuwa mchungaji wetu kwa kutufanya tulale chini (Zaburi 23:2). Punde tu uhusiano huo upo, Mungu hutuongoza kwenye maji tulivu, majani mabichi, nacho kikombe chetu hufurika. Tunaposimama tena, hayo majani mabichi hugeuka na kuwa ni ya rangi ya hudhurungi, maji huwa na tufani, nacho kikombe huwa kikavu.

Kifo ni mchungaji mwema akitufanya kulala chini katika mauti ili aweze kutupa majani mabichi ambayo hayawezi kubadilika na kuwa ya rangi ya hudhurungi, ilhali nayo maji tulivu hayatakuwa tufani, na kikombe hakitakuwa kavu. Ili kutupatia thamana hizi za uzima wa milele, ni lazima tuwe na ujuzi huu wa shida hizi ambazo hazina suluhisho yaani magonjwa na mauti. Haya ndiyo maelezo makuu na yakipekee kuhusu sababu ya dhiki kwa watu wake Mungu.

Neno lake Mungu linalo mengi ya kusema kuhusu dhiki, lakini ipo zaidi kwa watu wake Mungu na kwa sababu ambazo hatuzifahamu. Maneno ambayo sisi hutumia zaidi katika maisha haya ni, 'kwa nini?' Neno ambalo yamkini tutalitumia mno huko mbinguni lawezekana kuwa ni, 'Oh!' na baada ya kulitaja kwa miaka elfu kumi, tutaanza kusema, 'Haleluya!'

SURA YA TATU

KITABU CHA ZABURI

Kitabu cha Zaburi kinazungumzia mioyo ya watu wa Mungu wanapoabudu. Kuna Zaburi mia moja na hamsini zenye uvuvio, ambazo zilipata kuimbwa na watu wa Mungu katika Agano la Kale. Mungu aliwapa watu wake Zaburi ili kuwasaidia kueleza upendo, sifa, na maombi yao kwake Mungu wakati wanapoabudu. Hizi nyimbo zenye uvuvio zitakuvutia katika uwepo wake Mungu pamoja na kukusaidia kueleza upendo, sifa na maombi yako wakati unapomwabudu siku ya leo.

Mtazamo Wa Muhtasari Wa Zaburi

Kabla ya Agano la Kale kutafsiriwa kwa lugha ya Kiyunani, kitabu cha Zaburi kilikuwa kimegawany'wa katika sehemu tano tofauti: Zaburi 1-41, 42-72, 73-90, 91-107, na 108-150. Sura sabini na tatu zinasemekana kuwa za Daudi, kumi na mbili za Asafu, nao wana wa Kora kumi na moja. Wasomi wanaamini kwamba Hezekia aliandika zaburi kumi, Musa, Ezra pamoja na Sulemani moja kila mtu. Waandishi wa Zaburi nyingi hawafahamiki na yamkini kwamba baadhi yao walikuwa ni Walawi–wataalamu wa nyimbo waliochaguliwa na Daudi–au yawezekana kwamba Daudi mwenyewe ndiye mwandishi wa baadhi kati ya Zaburi ambazo hazina uhakika.

Uongozi Kuhusu Uimbaji

Maongozi ambayo mara kwa mara hutangulia zaburi ni maelekezo kwa mfano Nehilothi, ambayo huonyesha kufuatiwa na vyombo vya upepo, au Neginothi ambayo huonyesha vyombo vya nyuzi. Neno Sela, ambalo liko kwa wingi katika zaburi linamaanisha, 'tulia au zingatia kwa hali ya heshima kuhusu hilo.' Inawezekana kwamba maana yake ilikuwa jinsi ilivyo katika nyimbo zetu pale ambapo unashauriwa kupumzika kidogo. Wengi husema kwamba neno hilo liliashiria mahali vyombo vya muziki hucheza bila kutoa maneno.

Kwake Nani Na Kuhusu Nani

Waandishi wa zamani wa zaburi au hata wa siku hizi huzungumzia Mungu kuhusu yeye, ambako ni sifa; ilhali wakati mwingine huzungumza naye Mungu kuhusu mwanadamu, ambalo ni tendo la maombezi; au hata huzungumza naye Mungu wakati wote. Wao walizungumza na

mwanadamu kuhusu Mungu, kusema kwamba wao huwa wakihubiri. Unaposoma kila zaburi, hebu jiulize mwenyewe hivi, ‘Mwandishi anazungumza na nani, na ni kuhusu?’ Kuuliza na kuyajibu maswali haya kutakupatia nuru katika ibada yako ya kibinafsi na kufahamu vyema yale ambayo unahitajika kutenda katika zaburi hizo.

Hoja Zilio Katika Kitabu Cha Zaburi

Utapata hoja nne ambazo zinatiliwa mkazo katika Zaburi. Hoja inayotambulika zaidi ni kuhusu ‘Heri yule mtu.’ Hoja hii iko kwa wingi katika Zaburi. Heri mtu yule aliyebarikiwa. Zaburi hii hufafanua kwamba baraka zake yeye aliyebarikiwa sio kwa bahati mbaya, bali ni karamu ya matokeo ya imani na dhamana muhimu za kiroho kwake mwimbaji. Utaipata hoja hii imedhihirishwa katika Zaburi sura ya 1, 23, 32, 128, na kadhalika.

Hoja kuhusu hisia pia ni dhahiri katika Zaburi. Zaburi hizi zinahusika na hisia dhahiri na huwa zinatuoyesha njia bora ya kukumbana na hisia hizo. Haijalishi uko katika hali ya aina gani katika hisia zako unaposoma zaburi, wewe utakumbana na halki sawa na hiyo katika Zaburi. Ikiwa umeteswa, uko chini ya wingu la masumbuko ya kila aina, na umelemewa na mzigo wa hukumu au moyo uliovunjika, ikiwa wewe umejazwa na shukrani kwa wingi wa baraka zako, nawe unataka kueleza kuabudu kwa shukurani; haijalishi hisia ambayo uko nayo kwa kusoma zaburi, au kwamba kuna zaburi ambayo yazungumzia na kukuonyesha yale ambayo unahitaji kutenda kupitia hisia hizo.

Jaribu kutambua hatua aliyochukua mwandishi wa zaburi fulani kuhusu hali ya hisia ile nawe ufanye sawa na vile alivyotenda na hisia zako. Baadhi ya hisia zilio katika zaburi nyingine ziko katika Zaburi sura ya 3, 4, 32, 34, 51, na 55.

Ibada ni mojawapo ya hoja dhahiri ilio katika Zaburi. Katika zaburi za kuabudu, mwandishi hasemi tu kwamba anazungumza na Mungu kumhusu, bali anatuhimiza kuabudu na pia anatufundisha jinsi ya kuabudu. Baadhi ya zaburi za kuabudu ni sura ya 8, 63, 100, 103, na 107.

Waandishi wa Zaburi pia waliandika sawa na manabii, huku wakifanya zaburi ambazo zinajulikana kama za Kimasihi. Zaburi hizi zinazungumzia kwa njia ya unabii kuhusu kuja kwake Masihi. Daudi alizungumza kwa unabii kuhusu kuja kwake Yesu Kristo, pamoja na ufufuo wake katika Zaburi sura ya 16. Petro alihubiri kutoka zaburi hii siku ya Pentekoste. Mifano mingine kuhusu zaburi za kimasihi ni sura ya 2, 8, 46, 22, na 110.

Utangulizi Wa Kihistoria Wa Zaburi

Maelezo kuhusu utangulizi wa kihistoria wa zaburi mara kwa mara unapatikana katika Samweli wa Kwanza na wa pili na katika kitabu cha Mambo ya Nyakati. Daudi aliandika nusu ya zaburi, na hadithi kuhusu maisha yake inapatikana katika vitabu hivi viwili vya historia. Ujumbe pamoja na maelezo yalio katika utangulizi wa baadhi ya zaburi hizo huonyesha mseto wa historia hiyo. Kwa maelezo haya, unaweza kupata ushauri katika vitabu hivyo vya historia. Unapojifunza kuhusu maelezo ya utangulizi na historia kuhusu zaburi fulani, utapata usaidizi kwa kujumuisha na kutenda kulingana mafunzo yaliyo katika Zaburi ile.

Katika zaburi hizi, baadhi ya waandishi wake wanafanya maombi dhidi ya maadui wao. Katika maombi hayo, waandishi hao huomba Mungu awawezeshe kuwang'oa meno maadui wao kwa upanga, au kuwakatakata vipande kwa silaha zao. Hii ni kinyume na mafunzo yake Kristo kuhusu *'kuwapenda maadui wako na kuwaombea wale wenye kukutesa wewe'.*

Hii ni mojawapo ya sababu muhimu kuwa na mtazamo wa kihistoria wakati unaposoma Zaburi. Zaburi hizi za kale ziliandikwa wakati wa sheria ambayo iliwafunza kwamba ni sawa kuwachukia maadui, hasa waliomkosea Bwana. (Kumbukumbu la Torati 23:3-6). Kwa hivyo, Daudi hakuona pingamizi lo lote wakati wa maombi yake, *'Je, mimi siwachukii wale wenye kukuchukia wewe? Mimi nawachukia wao kwa chuki kamilifu na kwa upanga wangu mimi nitawapiga na kuwafanya mavumbi ya ardhi.'* Mtazamo wa kihistoria unathibitisha kwamba maombi haya yalikuwa sawa wakati yalipokuwa yakitendeka.

Zaburi Ya Ishirini Na Tatu

'Mazungumzo Ya Kondoo.'

Zaburi ya Daudi ya mchungaji inapendwa sana na ni sura yenye kuvutia sana katika maandiko kwa mamilioni ya Wayahudi, Wakatoliki na Waprotestante. Katika zaburi hii, Daudi alikuwa akihubiri kwa kuwa yeye alikuwa akizungumza na mwanadamu kuhusu Mungu. Mfumo wa uandishi

wa zaburi hii ni ‘mazungumzo ya kondoo’ kwa kuwa kondoo ndiye anena na kondoo wengine kuhusu ukuu wake Mchungaji:

‘Bwana ndiye mchungaji wangu,
Sitapungukiwa na kitu.
Katika malisho ya majani mabichi hunilaza,
Kando ya maji ya utulivu huniongoza.
Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza
Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.
Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti,
Sitaogopa mabaya;
Kwa maana Wewe upo pamoja nami,
Gongo lako na fimbo yako vyanifariji.
Waandaa meza mbele yangu,
Machoni pa watesi wangu.
Umenipaka mafuta kichwani pangu,
Na kikombe changu kinafurika.
Hakika wema na fadhili zitanifuata
Siku zote za maisha yangu;
Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.’

Zaidi ya kuwa zaburi yenye mahubiri, zaburi hii ya ishirini na tatu ni ya mtu aliyebarikiwa au mwenye heri. Katika zaburi zote za mwenye kubarikiwa, baraka zake ni za masharti. Katika zaburi hii, baadhi ya baraka zake Daudi ni majani mabichi, maji matulivu na kufurika kwa kikombe chake. Masharti ambayo yanaambatana na baraka hizo yanapatikana katika maneno yanayotangulia katika zaburi hii: *‘Bwana ndiye mchungaji wangu.’* Baraka zote ambazo Daudi anaorodhesha katika zaburi hii kwa wimbo wa mchungaji zilitokana na ushuhuda wake kwa Mungu wakati angesema kwamba Bwana ndiye mchungaji wake.

Majani mabichi ni mfano wa baraka za kimwili. Wakati Daudi anapozungumza kuhusu kikombe chake ‘kinafurika’ (5), anatumia mfano ambao unawakilisha furaha. Yeye ni mtu mwenye furaha. Je! Chanzo cha furaha yake ni kipi? Bwana ndiye mchungaji wake Daudi. Kila mara Bwana anapozidi kuwa mchungaji wake Daudi, yeye huwa na kila kitu anachohitaji–majani mabichi, maji matulivu, kikombe kinachofurika, meza iliyoandaliwa na kadhalika. Lakini baraka hizi zote zina

masharti. Zote zinatengemea uhusiano alio nao pamoja na mchungaji. Zaburi hii kwa hakika ni kuhusu uhusiano ulio muhimu sana katika ulimwengu–uhusiano wetu na Mungu.

Kuwepo Kwa Uhusiano

Tunapotambua jinsi uhusiano huo ulivyo muhimu, twahitajika kuuliza jinsi unaweza kutekelezwa. Jibu kwa swali hili letu linapatikana katika msitari wa pili wa zaburi hiyo: 'Hunilaza mimi.' Mchungaji huthibitisha uongozi wake juu ya kondoo kwa kumpiga kichwa kwa fimbo na kumwambia, 'lala chini!' Wakati mwingi Bwana hufanyika kuwa mchungaji wetu kwa kutugonga kwa fimbo kichwani kwa shida ambayo hatuwezi kuiepuka au kulitatua.

Uhusiano Katika Matendo

Ni baada tu ya Bwana kufanyika mchungaji wetu anapoweza kutuongoza. Na kwa sababu kondoo hunywa maji yaliyo tulivu kama bilauri, maji hayo huwakilisha tukio au mahali ambapo panakubalika kwetu. Mchugaji wetu mkuu hawezi kutuongoza katika sehemu hadi tujilaze chini na kukiri hoja mbili: kwamba Mungu ndiye mchungaji wetu na kwamba sisi tu kondoo. Mistari ifuatayo inatueleza uhusiano huu ukiwa vile unavyohitajika kuwa. Hii inamaanisha tuamke na kumwomba mchungaji ili uhusiano wetu uhuishwe tena.

Uhusiano Bora

Wakati Daudi anapohuzisha uhusiano huu mahala unapostahili, anatupatia maelezo ya kuvutia sana katika Biblia kuhusu uhusiano huo kati ya Mungu na binadamu. Yeye anatueleza kwamba haijalishi pale mchungaji atapomwongoza, yeye anafahamu kwamba mchungaji huyo atakuwa pamoja naye, atatembea mbele yake, naye atamfuata nyuma huku akiwa na upendo na wema usio na masharti ye yote ya kukutana na mahitaji yake, kumwagia baraka zake juu yake, na kukifanya kikombe chake kufurika. Yeye pia anafahamu kwamba uhusiano huu utaendelea siku zake zote za maisha–hata milele!

Ufanye ujumbe huu wa Zaburi ya ishirini na tatu kuwa sehemu ya maisha yako. Labda unaweza kukumbuka wakati ulimfanya Bwana kuwa mchungaji wako. Ulipata malisho katika majani mabichi na kando ya maji matulivu, nacho kikombe chako kilifurika kwa baraka zake. Je! Nyasi

zimegeuka na kuwa rangi ya hudhurungi au je, kikombe chako kimekuwa kavu? Je! Wewe umepotelea mbali na maji tulivu kwa kuwa umechagua kuwa mchungaji wa maisha yako mwenyewe?

Tambua kwamba unahitaji kuhuishwa. Mruhusu Mungu kuweka uhusiano wako vyema, na kuuweka mahali pema kwa ajili ya jina lake mwenyewe. Halafu, ishi ukifahamu kwamba mchungaji wako yu pamoja nawe, hutembea mbele yako, yeye hukufuata nyuma kwa wema na rehema zake, na kuiandaa meza ya mahitaji pamoja na kubariki maisha yako kwa upako wake, akijaza kikombe cha furaha iliyomo ndani yako. Ishi ukiwa na uhakika kwamba yeye anaweza kutenda hivyo siku zote za maisha yako. Tarajia uzima wa milele kwa tumaini lisiloweza kuzimwa, ukifahamu kwamba yeye anaweza kutenda hivyo milele!

Zaburi Ya Kwanza

Mtu Aliyebarikiwa.

Zaburi ya kwanza ina maelezo maelezo kuhusu mtu aliyebarikiwa. Zaburi nyingine kuhusu mtu aliyebarikiwa hufuata mfano wa zaburi ya kwanza, na kutuonyesha kwamba mtu aliyebarikiwa na kwamba baraka yake sio kwa bahati au nusra njema, bali ni kwa matukio ya uamuzi wake wenye kulingana na ushawishi pamoja na uchanguzi wake. Zaburi hii ya kwanza inasema hivi:

‘Heri mtu yule asiyekwenda
Katika shauri la wasio haki;
Wala hakusimama katika njia ya wakosaji;
Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.
Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo,
Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.
Naye atakuwa kama mti uliopandwa
Kandokando ya vijito vya maji,
Uzaao matunda yake kwa majira yake,
Wala jani lake halinyauki;
Na kila alitendalo litafanikiwa.
Sivyo walivyo wasio haki;
Hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo,

Kwa hiyo wasio haki hawatasimama hukumuni,
Wala wakosaji katika kusanyiko la wenye haki.
Kwa kuwa Bwana anaijua njia ya wenye haki,
Bali njia ya wasio haki itapotea.'

Ni Nani Mtu Aliyebarikiwa?

Zaburi ya kwanza inatambulisha watu wawili–mtu ambaye amebarikiwa na mwingine muovu. Zaburi hii inatumia mfumo wa mashairi ya Kiebrania ambao unataja ukweli kwa kunena maneno kwa kinyume. Daudi anatupatia maelezo kuhusu tabia yake mtu aliyebarikiwa kwa kumwonyesha yule ambaye si yeye. Kwa mfano, mtu aliye barikiwa *'hatembei katika shauri la wasio haki'* (1a), maanake kwamba yeye hutembea katika shauri la Mungu. Yeye hupata mashauri ya Mungu katika neno lake Mungu, ambapo *'huitafakari mchana na usiku.'* (2b).

Pia huyu mtu aliyebarikiwa *'haketi barazani pa wenye mizaha.'* (1). Maneno haya ya kupinga yanatueleza kwamba mtu aliyebarikiwa huketi katika kiti cha mwaamini–yeye ni mtu aliyeamini. Analiamini Neno lake Mungu na *'hupendezwa na sheria yake Bwana.'*(2a). Yeye anafahamu kuwa ufunguo wa kulifanya neno la Mungu kuwa na uwezo mkuu katika maisha yake ni kkwa kilitii Neno hilo. Hutembea katika mashauri ambayo anayapata katika Neno lake Mungu.

Zaburi hii iliandikwa na Daudi, ambaye alikuwa mfalme wa pili wa Israeli, na aliye bora zaidi katika historia yote ya Israeli. Kulingana na sheria yake Musa, ulikuwa ni wajibu wake mfalme kunakili kwa uangalifu nakala ya sheria na kuwa nayo kila mahali: *'Na awe nayo, asome humo siku zote atakazoishi; ili apate kujifunza kumcha Bwana, Mungu wake, ayashike maneno yote ya torati hii na amri hizi, kwa kuyafanya.'* (Kumbukumbu la Torati 17:19). Kulingana na Zaburi ya kwanza tunaposoma katika zaburi hizi zenye uvuvio, tunaweza kukubaliana kwamba nidhamu ilimfanya Daudi kulipenda Neno lake Mungu, nao upendo huu wa neno ulimfanya kuwa mtu aliyebarikiwa.

Baraka zake mtu aliyebarikiwa ni zipi? Baada ya kueleza ushawishi na uamuzi ambao ni sharti katika kuongoza kwa baraka zake mtu aliyebarikiwa, Daudi anaorodhesha baraka hizo:

Uthabiti.

Mtu aliyebarikiwa ni *'kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji'* (3a), ambapo udongo wake ni mwepesi na mizizi yake huwa mingi na yenye kina kuu. Mizizi yake inaenea pande zote. Lori kubwa linapougonga mti mkubwa, huwa linaharibika ilhali mti hautikiswi hata kidogo. Ni uthabiti na namna hii–uthabiti wa mti uliopandwa vyema na ulio na malisho bor –ambao hudhihirisha tabia yake mtu aliyebarikiwa. Yesu alisema jambo sawa na hili wakati alipotoa mfano kuhusu mtu aliyesikia na kutenda mafundisho yake (Mathayo 7:24, 25).

Rotuba.

Mtu aliyebarikiwa huwa na uzao mwingi–mti ambao unaeleza tabia yake *'huzaa matunda yake kwa majira yake.'* (3b). Hii inamaanisha kwamba kwa majira yake yote ya maisha, yeye huzaa matunda yanayoambatana na majira yaliyomo katika maisha yake. Kwa kuwa yeye anaamini na analipenda Neno lake Mungu, ufahamu wake kuhusu Mungu ni zaidi ya ule ulio katika kurasa takatifu na wenye kuzidi hadi uhusiano na Neno linaloishi. Uhusiano huu ndio ufunguo wa uzalishaji mkuu wake. Yesu alifundisha kwamba ni lazima tukae ndani yake jinsi tawi hukaa pamoja na mzabibu ikiwa tunahitaji kuzaa matunda mengi.

Maisha Marefu.

Mtu aliyebarikiwa hajifanyiki kuwa mwenye uchungu mwingi, au mzee aliyenyauka katika miaka yake ya uzeeni. Tunasoma kwamba, '*Jani lake halinyauki.'* Yeye hutukumbusha maneno yake mwandishi wa shairi hili: 'Zeeka pamoja nami. Wema waja siku za usoni. Ya mwisho iwe kwanza.' Kila siku apatao kuishi humtayarisha kwa kila siku ambayo hatapata kuishi. Thamani ya maisha yake hufanyika kuwa bora na bora zaidi jinsi anavyozidi kwa umri wa miaka katika maisha yake.

Mafanikio

Tunaendelea kusoma kwamba *'kila alitendalo, hufanikiwa'* (3b). Daudi alikuwa hapa hazungumzii kuhusu fanaka ya mali, bali fanaka ya kiroho. Kwa sababu vitabu vya mashairi hutilia mkazo utu wa ndani zaidi kuliko utu wa nje, hivyo basi tunaweza kusema kwamba ufanisi wake mtu aliyebarikiwa ni ufanisi wa utu wa ndani ambao pia huigusa thamana ya uzima wa milele. Cho chote

kile tutakachoacha nyuma wakati tutakapoondoka katika ulimwengu huu ni chakutamanika kuwa nacho tungalipo katika ulimwengu huu.

Usalama

Baraka inayotajwa kuwa ya mwisho yake mtu aliyebarikiwa pia inazungumziwa kwa kinyume*: 'Kwa hiyo wasio haki hawatasimama hukumuni, wala wakosaji katika kusanyiko la wenye haki.'* (5). Mtu aliyebarikiwa ana usalama katika maisha haya na yale yajayo kwa kuwa yeye hutembea kulingana na shauri ambalo yeye hulipata katika Neno lake Mungu. Yeye atasimama katika kazi iliyomalizwa yake Kristo katika hukumu naye ataungana na kundi la wenye haki milele kwa kuwa yeye hutenda. Jinsi baraka zinavyotajwa katika zaburi ya mchungaji, baraka ya mtu aliyebarikiwa katika zaburi ya kwanza ni *'siku zote za maisha yake na milele!'*

Watu Wawili walioketi Kwe Kiti, Wewe Ni Yupi?

Daudi anaeleza kuhusu mtu asiye haki kwa kuandika hivi, *'Sivyo walivyo wasio haki.'* (4a). Watu wasio haki hawaamini jinsi mwenye baraka anavyoamini. Wasio haki hawalifurahii neno lake Mungu, wala hawalitafakari Neno hilo mchana na usiku, na matokeo yake ni kwamba wao hawana uthabiti, rotuba, wingi wa siku, ufanisi au usalama, na hawataupata ujuzi wa uzima wa milele sawa na mtu aliyebarikiwa.

Ni kwa sababu gani mtu hubarikiwa? Ni kwa sababu ya uchan au hiari anaofanya mwenyewe. Yeye huchangua kuamini na kulitafakari neno lake Mungu, pamoja na kujitenga kutokana na wasio haki pamoja na njia zao ambazo hazizai matunda. Baraka zake ni karamu ya matokeo.

Changa moto kwa kila mwenye kubarikiwa ni: 'Watu wawili walioketi kwenye kiti, wewe ni yupi?' Kwa neema yake Mungu, Je! Wewe ndiye aliyebarikiwa? Je! Wewe huketi katika kiti chake anayeamini? Je! Unaliamini neno lake Mungu? Je! unalitafakari mchana na usiku? Je! unatembea kulingana na Zaburi ya kwanza? Huo ndio ufunguo kwa baraka zake mtu aliyebarikiwa.

Zaburi Mia Moja Ishirini Na Nane

Aliyebarikiwa Ni Kila Mmoja?

'Heri kila mtu amchaye Bwana,
Aendaye katika njia yake.
Taabu ya mikono yako hakika utaila;
Utakuwa heri, na kwako kwema.
Mkeo atakuwa kama mzabibu uzaao,
Vyumbani mwa nyumba yako.
Wanao kama miche ya mizeituni
Wakiizunguka meza yako.
Tazama, atabarikiwa hivyo, yule amchaye Bwana.
Bwana akubariki toka Sayuni;
Uone uheri wa Yerusalemu siku zote za maisha yako;
Naam, ukawaone wana wa wanao.
Amani ikae na Israeli.'

Je! Kila Mmoja Amebarikiwa?

Watu wengi huweka alama ya kikomo baada ya neno la tatu katika zaburi hii kwa sababu wao huamini kwamba kila mmoja amebarikiwa. Hata hivyo, maandiko yanatueleza kwamba baraka zake aliyebarikiwa zina masharti: *'Heri kila mtu amchaye Bwana, Aendaye katika njia yake'* (1). Na ambavyo tumekuwa tukijifunza, mtu aliyebarikiwa, amebarikiwa kwa sababu ya ushawishi wa imani yake na uamuzi wake usio wa kulazimishwa.

Zaburi hufundisha kwamba kila mtu anayemcha Mungu amebarikiwa, lakini jambo hili huzoa swali lingine: Si kitabu chake Ayubu kilitufundisha kwamba Mungu huwabariki wakati wote watu walio wema? Wakati marafiki wake Ayubu walipomwambia kwamba Mungu huwaadhibu wale wenye kutenda dhambi na kuwabariki wale wasiotenda dhambi, Mungu aliwaambia kwamba wao walikuwa wamekosea. Hata hivyo, tunaweza kujifunza kutokana na zaburi yake mtu aliyebarikiwa kwamba mtu aliyebarikiwa mara nyingi huvuna yale aliyoyapanda, na wakati watu wema kama Ayubu wanapokuwa katika dhiki, hilo si jambo la kawaida.

Mpango Wake Mungu

Zaburi 128 inatufundisha kwamba mtu aliyebarikiwa, baraka zake hutoshea katika mipango yake Mungu ili kuufikia ulimwengu. Jinsi tulivyojifunza katika Ayubu, jambo ambalo linahitajika kutoka kwetu tuliobarikiwa sio 'Bwana, ni kitu gani ambacho utanipatia?' ila ni 'Bwana, je, kubarikiwa kwangu kunaweza kukufaidi vipi?'

Mpango wake Mungu huwa na utaratibu fulani. Yeye humtafuta mtu ambaye ataamini na kumtii, na huchagua kumbariki (1-2). Baraka yake Mungu hupitia kwake yule mtu hadi kwa mkewe, naye *mkewe huwa kama mzabibu uzaao vyumbani mwa nyumba yake* (3a). Kisha baraka ile hupitia kwa mtu yule na mkewe mwenye rotuba hadi kwa wanao, ambao tunasoma kwamba hufanyika *'kama miche ya mizeituni wakiizungukia meza yako''* (3b). Mmea wa mzeituni ni ishara ya rotuba yenye uzao.

Baraka zake Mungu hupita katika jamaa ndogo hadi kuibariki Sayuni, ambayo ilikuwa jamii ya kiroho katika Agano la Kale. Kupitia kwa jamii ya kiroho (Sayuni), baraka yake Mungu katika jamaa ile huugusa mji (Yerusalemu), taifa (Israeli), na baadaye ulimwengu wote. Zaburi hii kwa hakika hufundisha kwamba Mungu huitumia jamaa ndogo ili kuueleza ulimwengu kuhusu yeye mwenyewe. Anapogusa mji, taifa, pamoja na ulimwengu, Yeye huanza na mtu aliyebarikiwa pamoja nayo jamaa yake.

Zaburi ya Mia moja na Ishirini na Saba

Thamana Zake Mungu.

'Bwana asipoijenga nyumba
Waijengao wafanya kazi bure.

Bwana asipoulinda mji s
Yeye aulindaye akesha bure.
Kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema,
Na kukawia kwenda kulala,
Na kula chakula cha taabu;
Yeye humpa mpenzi wake usingizi.
Tazama, wana ndio urithi wa Bwana,

Uzao wa tumbo ni thawabu.
Kama mishale mkononi mwa shujaa,
Ndivyo walivyo wana wa ujanani.

Heri mtu yule

Aliyelijaza podo lake hivyo.
Naam, hawataona aibu
Wanaposema na adui langoni.'

Zaburi hii fupi, ambayo yahitajika kutambulikana kama mwenzi wake zaburi ya 128. Ndio zaburi tu iliyoandikwa na Sulemani. Kwa yeye alikuwa ni mjenzi mkuu, tunaweza kutarajia yeye kutumia lugha ya mfano katika zaburi hii. Yeye ndiye aliyekuwa mjenzi mkuu wa Hekalu lililopewa jina lake; alijenga miji, bustani na zizi za farasi pamoja na marekebu nyingi. Hata hivyo, Sulemani anatuambia kwamba inawezekana kufanya ujenzi kwa ubatili mtupu: *'Bwana asipoijenga nyumba Waijengao wafanya kazi bure.'* (1). Yeye anatuambia kuwa inawezekana kujenga bure, au kujenga vitu vibaya.

Zaburi hii inafanana na maneno yake Sulemani ya mwisho yenye hekima anayokiri katika kitabu cha Mhubiri, mahali alipohubiri kwamba mengi ya yale aliyojenga katika maisha yake yalikuwa ni ubatili mtupu. Anapotoka katika mfano wake wa ujenzi hadi wa wanawe, anawaambia wazazi kwamba jambo la muhimu sana ambalo wanaweza kufanya maishani mwao ni kuyajenga maisha ya wanao. Yawezekana kwamba Sulemani alikuwa akitueleza kuwa alijuta kwamba angalitumia muda mwingi kuyajenga maisha ya wanawe badala ya mambo mengine aliyokuwa akiyajenga.

Sulemani anatuambia kuwa: *'Kama mishale mkononi mwa shujaa, ndivyo walivyo wana wa ujanani.'* (4). Mishale katika lugha hii ya mfano ni wanao ilhali wewe ndiwe upinde. Mwelekeo na uwezo ambao wanao wataelekea katika ulimwengu huu utategemea upinde utakaotumia dhidi yao hapa duniani. Upinde huo ni nyumba yako.

Ujumbe mkuu katika Zaburi hii unapatika katika maneno ya kufungua ambayo yanasema hivi: *'Bwana asipoijenga nyumba waijengao wafanya kazi ya bure.'* Yapo mambo mengi ambayo ni Mungu pekee awezaye kufanya. Ni Mungu peke yake awezaye kutengeneza maisha upya ndani ya wanao. Ni Mungu peke yake awezaye kuwapa karama ya imani. Na kwa njia nyingine, Mungu hawezi kuyajenga maisha ya wanao hadi wewe umruhusu kufanya hivyo. Ukweli huu upo katika kifungu cha

usemi wenye kuvutia sana. Sulemani anatuambia hivi, *'Yeye humpa mpenzi wake usingizi.'* Wakati sisi tungali macho, Mungu hawezi kutupatia nguvu mpya katika miili yetu. Lakini, tunaponyamaa na kulala usingizi, Mungu huchukua fursa ya kuweka nguvu na maisha mapya katika miili yetu. Utumie usemi huu katika nyadhfa na changa moto kama wazazi.

Maana Yake Ni Nini?

Inawezekana kusumbuka, kufanya kazi, na pia kufanya ujenzi kwa kuwa thamana zetu ni mbovu. Zaburi hii ni changa moto kwetu sisi kuzeweka rasilmali zetu kwa wazazi kwa kuwa ni kupitia jamaa ambapo Mungu hufikia ulimwengu. Ni vyema kama tukijitolea wenyewe kwa thamana hizi kwa kuwa Shetani anafahamu kwamba Mungu huzitumia jamaa kuufikia ulimwengu. Shida za ndoa pamoja na kuvunjika kwa jamii nyingi ni ushahidi tosha kwamba ibilisi anajitahidi kuivunja kazi hii muhimu yake Mungu kwa kuzikata kamba pinde zetu.

Je, kila mmoja wetu amebarikiwa? Hii si kulingana na kile ambacho tumejifunza katika mtu aliyebarikiwa katika zaburi. Ni mtu yule mwenye utiifu na kuamini anayebarikiwa awe mke au mume, nazo baraka zake huugusa ulimwengu kupitia watoto wao. Je, wewe ndiye mwanamume au mwanamke huyo? Tazama hali ya mtu aliyebarikiwa kisha ulijibu swali hili: 'Watu wawili wameketi kwenye kiti, wewe ni yupi?'

Zaburi Ya Nne

Suluhisho Kwa Kusongwa

Baada ya kutilia maanani baadhi ya zaburi zake mwenye kubarikiwa, sasa tuko tayari kutilia maanani baadhi ya zaburi zinazotajwa kama za hisia. Mara kwa mara zaburi hizi ni kuhusu maombi, pale ambapo mwandishi au mwimbaji wake huzungumza na Mungu kumhusu mwanadamu–mara mwingi kujihusu mwenyewe. Mojawapo ya zaburi hizo ni ya nne:

'Ee Mungu wa haki yangu, uniitikie niitapo;
Umenifanyizia nafasi wakati wa shida;
Unifadhili na kuisikia sala yangu.
Enyi wanadamu, hata lini utukufu wangu utafedheheka?

Je! Mtapenda ubatili na kutafuta uongo?
Bali jueni ya kuwa Bwana amejiteulia mtauwa;
Bwana atasikia nimwitapo.
Mwe na hofu wala msitende dhambi,
Tafakarini vitandani mwenu na kutulia.
Toeni dhabihu za haki,
Na kumtumaini Bwana.
Wengi husema, Nani atakatuonyesha mema?
Bwana, utuinulie nuru ya uso wako.
Umenitia furaha moyoni mwangu,
Kupita yao wanapozidishwa nafaka na divai.
Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara,
Maana Wewe, Bwana, peke yako,
Ndiwe unijaliaye kukaa salama.'

Je! Unaweza kukumbiliana na msongamano wa kimaisha kwa njia ipi? Mazingira yake mwandishi wa Zaburi ya Nne ni ya kusongwa. Mwandishi kwa hakika anazungumzia kuhusu kusongwa kimaisha. Ulimwengu huu tunaoishi siku ya leo ambao ni wa kusongwa unafahamika kama 'kizazi cha usumbufu.' Zaburi hii inatuonyesha jinsi ya kukumbiliana na kusongwa kwa kila siku.

Maombi

Katika Zaburi ya Nne, Daudi alikambiliana na kusongwa kwa hisia zake kupitia maombi. Aliomba hivi: *'Ee Mungu wa haki yangu, uniitikie niitapo'* (4). Maombi ni mazungumzo pamoja na Mungu. Mazungumzo huwa kwa hali mbili–kuzungumza na kusikiliza. Mungu anataka wewe uzungumze naye, lakini pia anataka kuzungumza nawe. Katika Zaburi nyingi za maombi, kwanza tunamwona mwimbaji akizungumza naye Mungu, na baadaye tunamsikia Mungu akimjibu. Mwimbaji anafanya maombi na baadaye anapokea hakikisho kwamba Mungu ameyasikia maombi yake kwa kuwa Yeye huyajibu.

Daudi alianza ombi hili akimwambia Mungu kina cha kusongwa kwake (2). Mungu alimjibu kwa kumpatia ufunuo: *'Bali jueni ya kuwa Bwana amejiteulia mtauwa; Bwana atasikia nimwitapo. Mwe na hofu wala msitende dhambi.'*(3, 4a). Wakati Mungu anapoyajibu maombi yetu, hatuhitajiki

kuwa watu wa kawaida tena. Hebu fikiria maana yake kuwa na maombi yaliyojibiwa. Hii inamaanisha kwamba Mungu wa ulimwengu mzima anashughulika nasi, hutusikia na kutujibu wakati tunapozungumza naye. Punde tu tunapoupata ushuhuda wa maombi yaliyojibiwa, maisha hayatakikani kuwa kama yalivyokuwa hapo awali.

Uchunguze Moyo Wako

Wakati Mungu alipozungumza na Daudi, alimwambia afanye jambo fulani: *'Tafakarini vitandani mwenu na kutulia'* (4b). Wakati Mungu alipomwambia Daudi kutulia, alikuwa akimwambia amsikilize. Inawezekana kwamba wakati Mungu alipomwambia Daudi *'Tafakarini vitandani mwenu,'* alikuwa akimwambia azungungumze na moyo wake. Alimtaka Daudi kuuchunguza moyo wake, au kuwa na mkutano mdogo na nafsi yake.

Tenda Lililo Jema

Daudi alipouchunguza moyo wake, Mungu alimwonyesha jambo la kutenda kuhusu kusongwa kwake. Mungu alimfanya Daudi kufahamu kwamba alitakikana, *'kuzitoa dhabihu za haki, Na kumtumaini Bwana'* (5). Kwa sababu gani alihitaji kutenda hivi? Kwa maana wengi walikuwa wakimtazama na kuuliza*, 'Nani atakayetuonyesha mema?'* (6a). Watu walikuwa wakimtazama Daudi. Wao walikuwa wakijifunza kuhusu Mungu kutoka kwa mfano wake Daudi.

Tunaweza kusema kwamba Daudi alikumbana na swala ambalo lilihitaji kukata shauri lake mwenyewe. Yeye angelitenda jambo la haraka na kuepuka. Au, angelitenda lililo jema. ama angelitenda lililo jema, yeye aliamini kwamba hangeliweza kuepukana na matokeo ya kusongwa kwake. Na kwa kuwa yeye alikuwa mtu mwenye stahi, hangeliweza kuishi na dhamira yake kwa kulitenda jambo la kuepukana na shauri lake. Baada ya kuyafanya mazungumzo pamoja naye Mungu, yeye aliamua kulitenda lililo jema. Yeye alifahamu kwamba watu walikuwa wakilitafuta lililo jema, maanake kulitenda lililo jema hata kama ni kwa gharama kuu.

Wakati Daudi aliufanya uamuzi wake wa kuzitoa dhabihu za haki, yeye aliupata ujuzi wa kuzibadilisha hisia zake. Alisema hivi, *'Umenitia furaha moyoni mwangu. . . Katika amani nitajilaza na kuupata usingizi mara, Maana Wewe, Bwana, peke yako, Ndiwe unijaliaye kukaa salama'* (7a, 8).

Kama hali yako ya ihisia inalingana na ya Daudi katika kusongwa, tafakari moyoni mwako na uwe na mazungumzo pamoja na Mungu. Kama usumbufu wake waweza kuonekana kuwa ulitokana na pingamizi ya kiroho, kilicho rahisi na cha kuepukana na kile kilicho chema, ufanye uamuzi moyoni mwako kuzitoa dhabihu za haki, na uliweke tumaini lako kwake Mungu. Thibitisha kwamba suluhisho lake Daudi kwa kusongwa linaweza kuzibadilisha hisia zako kutoka kwa uvuto wa kilicho chema, usumbufu, na woga, hadi katika hali ya kihisia yenye kupumzika kutokana na kutumainia, amani, na usingizi mnono na mzuri.

Zaburi Mia Moja Thelathini Na Tisa

Mshauri Mkuu

'*Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele.'* (Zaburi 139:23,24).

Huu ni mfano mwingine kuhusu zaburi ya maombi, ambapo mwandishi huyu mwenye uvuvio anazungumza na Mungu kumhusu mwanadamu. Ni maombi makuu yake Daudi katika Zaburi ya mia moja thelathini na tisa. Katika zaburi hii, twampata Mungu kuwa Mshauri Mkuu wake Daudi. Wakati Mungu alipomwambia Sauli kupitia Samweli kwamba alikuwa amempata yule atakaye kuchukua mahala pake pa mfalme wa Israeli, Mungu alimwelezea Daudi kama mtu anayetafuta moyo Wake, na ambaye angelitenda mapenzi yote yake Mungu. Kwa sababu Daudi alitaka kutembea katika mapenzi yake Mungu maishani mwake, aliomba maombi maombi haya yenye kuvutia sana. Kina cha maombi haya kimetiliwa mkazo vyema katika mistari miwili ya mwisho. Tukigawa Zaburi hii katika sehemu mbili, kila sehemu itatuonyesha ni nani huyo Mungu ambaye Daudi alimwomba ombi hili–na kwa sababu gani anayaelekeza maombi yake kwa huyu Mungu. Wakati Daudi alipoliomba ombi hili, kulikuwa na miungu wengi na sanamu ambazo maombi mengi yalielekezwa kwao.

Katika sehemu ya kwanza (1-5), Daudi anatueleza kwamba anaomba maombi yake kwa Mungu ambaye anamfahamu. Ufahamu wake Mungu kumhusu Daudi hauna kipimo. Daudi aliomba: *'Ee Bwana, umenichunguza na kunijuA'* (1). Unaweza kusema kwamba unamfahamu mtu mashuhuri, na labda ni kiongozi wa kisiasa katika nchi yako. Hata hivyo, je! Si ingelikuwa jambo la kupendeza

zaidi kama yule mtu mashuhuri angelisema mbele ya umati kwamba anakufahamu wewe? Daudi anapendezwa na ukweli kwamba Mungu wa ulimwengu mzima anamfahamu yeye!

Unapoutafuta ushauri wake mwanadamu, unafaa kufahamu kuwa ni wa kiwango kidogo kinacholingana na yale utakayowaeleza kujihusu wewe mwenyewe. Haijalishi wamehitimu kiasi gani, uwezo wao kukusaidia unalingana na yale utakayowaeleza kuhusu historia yako pamoja na tatizo lililopo kwa wakati huo. Lakini Mungu anakufahamu vyema kabisa. Anafahamu mawazo yako hata kabla wewe kuyafikiria, naye *'ameelewa na njia zako zote.'* (3b).

Sehemu ya tatu (13-16) inaonyesha Daudi akiomba Mungu aliyemuumba. Daudi alimzungumzia Mungu kwa kusema, *'maana Wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu, uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ni ya ajabu, Na nafsi yangu yajua sana, Mifupa yangu haikusitirika kwako, Nilipoumbwa kwa siri, Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi; Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; chuoni mwako ziliandikwa zote pia.'* (13-16b). Kabla sisi kuwepo, Mungu alikuwa ameorodhesha siku zetu chuoni mwake. Hebu tafakari juu ya haya unapoorodhesha mipango yako ya siku, juma na miezi katika kalenda yako kwa mwaka mzima. Hii pia inamaanisha kwamba hakuna jambo kama ajali ya mwanadamu. Sisi sote huishi kwa hiari na mfumo wake Mungu. Hebu tafakari juu ya haya unapofikiria kuitoa mimba.

Sehemu ya nne (17,18), inaonyesha kwamba Daudi alikuwa akielekeza maombi yake kwa Mungu ambaye hufikiri kuhusu yeye. Twajifunza kutoka kwake Daudi kwamba fkira za Mungu zina thamani nyingi na kwamba hazina hesabu au kipimo (17). Njia muhimu sana kuhusu uhusiano wa karibu ni kumwambia mpenzi wako kwamba unafikiri juu yake kila mara. Mungu hufikiri juu yetu zaidi kuliko tunavyojifikiria wenyewe.

Mwishowe, Daudi anaelekeza maombi yake kwa Mungu ambaye ni mlinzi wake (19-22). Ni katika hali hii ambapo anamwomba Mungu kuwaangamiza maadui zake. Yeye anaomba maombi ya ulinzi kwa ujasiri mkuu kwamba Mungu atamsaidia kuwaangamiza maadui zake.

Baada ya kuthibitisha tabia ya Mungu anayemwomba, Daudi anataja kusudi la maombi yake wakati anapomsihi Mungu 'kumchunguza' na 'kumjaribu' aone kama iko njia iletayo majuto ndnai

yake (23, 24). Yeye alifanya sala hili kwa Mungu ambaye hawezi kumtoroka, kwa Mungu ambaye anamfahamu, na kumuumba, anayemfikiri na ambaye atamlinda.

Huyu ndiye Mungu ambaye twamwelekezea maombi yetu yote. Wakati hauna uhakika kuhusu nia za moyo wako, lakini unataka kutembea katika njia ya milele ya mapenzi yake Mungu katika maisha yako; basi karibia kiti cha mshauri mkuu ambaye Daudi alimwomba. Mwulize Yeye kukitoa kifuniko juu ya moyo wako na kukuonyesha mambo ambayo hayahitajiki ndani ya moyo wako. Mwulize Yeye kukitoa kifuniko kilichoko katika nia yako na kukuonyesha mawazo ambayo hayatakikani kuwepo kwa kuwa unataka kutembea katika njia ya milele ya mapenzi kamili katika maisha yako.

Zaburi Mia Moja

'Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote;
Mtumikieni Bwana kwa furaha;
Njoni mbele zake kwa kuimba;
Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu;
Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake;
Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru;
Nyuani mwake kwa kusifu;
Mshukuruni, lihimidini jina lake;
Kwa kuwa Bwana ndiye mwema;
Rehema zake ni za milele;
Na uaminifu wake vizazi na vizazi.'

Zaburi mia moja ni maelezo kuhusu kuabudu. Inatueleza maana ya kuabudu. Kuabudu ni kuja mbele ya uwepo wake Mungu. Kuna uwepo wake Mungu, na kufikia kwenye uwepo huo ndicho kina kikuu cha Ibada. Katika Zaburi hii ya Daudi, yeye hafafanui tu kuhusu Ibada kwetu sisi, bali kupitia misemo yenye mifano, anatuonyesha jinsi ya kuabudu.

Katika nyakati za Agano la Kale, kulikuwepo na taratibu ambayo iliyofuatwa wakati mtu anapokuwa na mkutano pamoja na mfalme. Kitu cha kwanza alichofanya ni kuingia ndani ya malango ya kasri la mfalme. Na kama yeye alikuwa mfalme mkuu, basi yule mgeni angetembea

katika kinjia kilicho kwenye kasri hilo lenye askari walipiga safu pande zote mbili, kabla ya kuifikia milango mikubwa iliyokuelekeza ndani kuliko mfalme.

Kama mfalme, Daudi alikuwa anafahamu taratibu hii vizuri sana. Yeye alichangua taratibu hii ili kufafanua kuhusu ibada na jinsi ya kuifanya. Kulingana na Daudi, Ibada ni kusongea kwenye uwepo wake Mungu.

Kusongea kwenye uwepo wake Mungu kwahitajika kuanza katika 'malango ya shukrani' (4a). Twahitajika kuanza ushuhuda wetu wa kuabudu kwa kumshukuru Mungu kwa baraka zetu zote. Shukrani huzaa ibada. Moyo wenye shukrani ndiyo 'malango' ambayo hutuongoza katika uwepo wake Mungu.

Daudi anafafanua zaidi mifano katika usemi wake wakati anapoandika kwamba malango ya shukrani huongoza katika nyuani mwake kwa kusifu (4b). Tunapoanza ushuhuda wetu wa ibada kwa shukrani, huwa tunamsifu Mungu. Sisi husonga kutoka kumshukuru Mungu kwa sababu ya baraka zetu nyingi hadi katika kuzungumza naye Naye kumhusu na kumsifu. Tunapoyapita 'malango ya shukurani,' mkazo wetu unaelekea katika mkono wake Mungu ambao sisi hupokea kutoka kwake. Lakini tunapoingia nyuani mwa sifa zake, mwelekeo wetu unakuwa uso wake Mungu.

Kwa karne nyingi, wakongwe wa imani wametueleza kwamba mlango ambao hutuelekeza katika uwepo wake Mungu ni ule wa sifa. Katika usemi wake Daudi ulio na uvuvio, mlango huo unaotuongoza katika uwepo wake Mungu ni uimbaji. Daudi aandika hivi: *'Njoni mbele zake kwa kuimba.'* (2b). Alikuwa Daudi ambaye aliuleta wimbaji au muziki na ibada pamoja. Yeye alikuwa na Walawi elfu nne ambao kazi yao ilikuwa ni wimbaji tu pamoja na vyombo ambavyo Daudi mwenyewe alivijenga kwa kusudi hilo (1 Mambo ya Nyakati 23:5).

Kuna wakati katika maisha haya ambapo twahitajika kueleza kile kisichoweza kuelezeka. Hii ndiyo sababu wapenzi hubandikana majina ya utani ambayo baadaye huwapa aibu sana. Wao hujaribu kuueleza upendo wao unaotatanisha kwa mwingine. Shauku hiyo siyo kuu ikiwa tuko katika uwepo wake Mungu. Kulingana na Daudi, ni uimbaji ambao hufungua mlango wakutuingiza kwenye uwepo wake Mungu.

Tunapofika katika uwepo wake Mungu, twaweza kukufahamu kupitia ushuhuda yale yanayofahamika tu katika akili zetu. Jambo la kwanza, twafahamu kwamba Yeye kwa uhakika ndiye Mungu. Tunapomwabudu, sisi hukubali kwamba Bwana ndiye Mungu na kwamba tu kondoo wa malisho yake (3). Hili linawezekana kuwa ndilo Mtume Paulo aliyomaanisha wakati alipoandika kwamba, *'Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema, Yesu amelaaniwa; wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu.'* (1 Wakorintho 12:3).

Hivyo basi, sisi hufahamu katika ushuhuda wetu kwamba 'Mungu ni mwema.' Wakati mwingi tunakataa kujitolea wenyewe kabisa kwake Mungu kwa sababu badala ya kukiri, 'Bwana ni mwema,' huwa tunasema kwa matendo yetu kuwa, 'Mungu ni mbaya.' Zaburi hii inasema kwamba katika uwepo wa Mungu, sio kwamba tunafahamu Bwana ndiye Mungu, bali twafahamu pia kwamba 'Mungu ni mwema' (5a). Mapenzi yake Mungu kwetu ni bora kwa kuwa Yeye ni mwema.

Katika uwepo wake, twafahamu pia kwamba Yeye anataka watu katika kila kizazi kila mahali ulimwenguni waje katika uwepo wake na kufahamu yale tunayofahamu kwa sasa. Msitari wa kwanza kwa zaburi hii unamalizikia na maneno haya, 'dunia yote.' Nao msitari wa mwisho unamalizikia kwa maneno, 'vizazi na vizazi.' (5c). Wale ambao huabudu katika uwepo wake Mungu hufahamu kwamba Mungu hupendezwa na watu wakimfahamu Yeye. Biblia na historia ya Kanisa zimejaa hadithi za watu waliokuwa na ushuhuda wa maana wa kumjia Mungu ambao uliwaongoza katika maisha yenye mazao kwake Mungu.

Mfumo wa hali hii ya kuabudu unatajwa katika sentesi ya pili katika zaburi wakati tunapohimizwa *'Mtumikieni Bwana kwa furaha.'* Tunapomwabudu Mungu kwa ukweli, twamtumikia katika furaha, bali siyo kwa sababu ni jukumu letu kumtumikia. Katika zaburi hizi za kuabudu, tumejifunza ibada ni nini, na matokeo ya ushuhuda wa wokovu wa kweli katika ibada.

Zaburi Thelathini Na Nne

Maagizo Bora Kwake Aliyeshindwa.

Zaburi ya thelathini na nne ni mojawapo ya zaburi za hisia au maombi ingawa pia ni ya ibada na mahubiri. Maelezo ya mwanzo katika zaburi ya thelathini na nne yanatupatia utangulizi wa kihistoria katika zaburi hiyo. Zaburi hii inawakilisha kipindi cha giza katika maisha yake Daudi wakati alipokuwa akimtoroka Sauli wakati alipogeuka kuwa mtoro. Kipindi hicho cha giza katika maisha ya Daudi kinaelezewa katika 1 Samweli 21 na 22. Wakati Daudi alipomtoroka Sauli na kuwa adui mkuu wa watu, kwa usalama wake mwenyewe; alikuwa na wazo kwamba aungane na mfalme wa Wafilisti kupigana na Sauli. Wakati jaribio hilo lilipokosa kufua dafu, Daudi alifanyika kuwa mkimbizi na aliishi katika mapango huko nyikani. Baadaye, twasoma kwamba watu waliokuwa wemesongwa waliungana naye huko nyikani, na wale wenye madeni, na wale wasiotosheleka (1 Samweli 22:2). Kulingana na desturi ya siku hizo, kuwna na deni ilimaanisha kwamba uko hatarini kufungwa gerezani, kama ilivyoelezwa kwenye mfano alioutoa Yesu katika sura ya kumi na nane ya Injili ya Mathayo. Ni jambo la kushangaza tunapotambua kwamba huu ulikuwa mkutano wake Daudi na watu ambao walifahamika kama ‘mashujaa wa Daudi.’

Zaburi thelathini na nne ni mfano na ufupisho wa yale Daudi aliyohubiri kwa wakimbizi na watu waliokuwa wameshindwa, ambao walifanyika kuwa mashujaa kwa kuwa walifahamu na kuamini kina cha yale Daudi aliyowahubiria. Maagizo yake Daudi kwa kushindwa kwao yanaweza kufupishwa hivi, ‘Watu watatu wameketi kwenye kitini, je! Wewe ni yupi?’

Mtu Mwenye Matumaini

Mtu ambaye angali na tumaini huamini kwamba kuna kitu chema katika maisha haya na kwamba yeye atakipata. Mungu huiweka tumaini ndani ya kila moyo wa mwanadamu. Mungu huiweka tumaini ndani ya mioyo yetu kwa kuwa tumaini inaweza kutuongoza katika imani. Hii ndiyo sababu sura ya imani katika Biblia inaanza kwa kutueleza kwamba imani hutupa uhakika wa yale tunayotumainia. Ni imani ambayo hutuongoza kwake Mungu.

Nchini Marekani kila mwaka, kati ya takribani watu elfu ishirini na tano hadi elfu thelathini hujiua. Wakati madaktari wa mambo ya akili wanapoulizwa kutoa maelezo kuhusu ni sababu gani

watu hao hujiua hivyo, mojawapo ya majibu wanayotoa ni kwamba watu hujiangamiza wakati wanapopoteza tumaini. Wakati watu wanapokosa kuamini kwamba kuna jambo nzuri litakalotendeka kwao, wao huamua kujiuwa.

Ingawa ni pingo kubwa kwa idadi hiyo kati elfu ishirini na tano na elfu thelathini na tano kila mwaka huko marekani, je! Si ni jambo la kushangaza kuonyesha kwamba watu milioni mia mbili na hamsini wana matumaini huko Marekani? Tunalo tumaini kwa kuwa tunazaliwa nalo katika mioyo yetu. Kusudi lake Mungu ni kwamba tumaini analoliweka ndani ya mioyo yetu hutuongoza kwa imani, na ni kwa mapenzi kwamba imani yetu hutuongoza katika uhusiano pamoja naye.

Kulingana na mtume Paulo, thamana kuu na zenye kudumu katika maisha ni tumaini, imani na upendo (1 Wakorintho 13:13). Pendo ndilo kuu kati ya thamani hizi kwa kuwa upendo sio kitu ambacho hutuongoza kwa jambo lingine ambalo hutufikisha kwake Mungu. Tunaposhuhudia upendo huu ambao Paulo anazungumzia, huwa tumefika pale. Maneno, 'Mungu ni upendo' ambayo yanajulikana sana humaanisha kwamba kuna thamani ya upendo ambayo ni Mungu.

Mtu Asiye Na Tumaini (34:16, 21).

Kuna hali ya mtu kuwa bila tumaini kabisa. Mtu ambaye hutaka kilicho kinyume cha Mungu, hana tumaini kabisa. Ikiwa Mungu yuko upande wako, ni nani awezaye kuwa kinyume chako? Hata hivyo, ikiwa Mungu yuko kinyume chako, ni nani awezaye kukutetea? Mtume Paulo alikubaliana na walimu wa nyakati za zamani, kama Gamalieli, wakati alipoandika hivi, *'Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?'* Upande mwingine wa maneno haya pia ni kweli: 'Ikiwa Mungu yupo kinyume chetu, ni nani awezaye kututetea?' (Warumi 8:31; Matendo 5:34-40). Mtu ambaye huenda kinyume cha Mungu huelekea upande ambao hufanya maisha yake kuwa ukiwa na kukosa tumaini. Daudi aueleza ukweli huu anapoandika: *'Uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya . . .Uovu utamwua asiye haki.'* (16, 21).

Mtu Mwenye (Heri) Furaha (34:15, 17-20,22)

Usuhuda na utambulizi utatilia mkazo furaha na matokeo mema ya mtu mcha Mungu na maovu na kukosa furaha kwa mtu asiyemcha Mungu. Utambulizi huu ni wa kweli katika maisha haya. Kitabu chake Ayubu na maandiko mengine mengi yanakuonya wewe: 'Kutosema kila wakati' pamoja na kusema 'Haiwezekani kamwe!' (Tazama: Sababu Thelathini Kwa Nini Watu Wa Mungu Hupitia

Kwenye Dhiki' ambayo ni maelezo katika kitabu cha Ayubu yaliyo katika kitabu hiki.) Katika hali ya uzima wa milele, utambuzi huu utabaki kweli (Zaburi 73)!

Matokeo (34:3-8)

Daudi anawaeleza watoro hao walioshindwa kuhusu ushuhuda wake wa jinsi alivyotoka kwenye ukiwa wa kupoza tumaini, hadi kuifikia tumaini, kisha kuwa mtu mwenye furaha. Tambua maongezi haya ya Daudi ya kibinafsi*: 'Nalimtafuta Bwana… akanijibu… Akaniponya na hofu zangu zote. . . Maskini huyu aliita!… Bwana akasikia, akamwokoa na taabu zake zote.'* Huu ni ushuhuda wa kibinafsi kuhusu ujuzi wake wa wokovu.

Ushauri Wa Daudi Kwa Wenye Kushindwa

'Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema,' kisha ugundue kwamba mtu yule ambaye anatumaini kwa Mungu amebarikiwa. (8). Kwa kupitia ushuhuda wa kibinafsi wa wokovu, tambua kwamba Bwana alitumainia kuwa na ujuzi wake katika maisha haya.

Maagano Kati Ya Daudi na Watu Wake Mashuhuri

'Mtukuzeni Bwana Pamoja nami, Na tuliadhimishe jina lake pamoja.'(3). Maagano haya ni maelezo ya kuvutia ya kiroho katika jamii. Huu ndio mfano wa mahubiri ambayo yaliwafanya watu mashuhuri wake Daudi. Usisahau kwamba walikuwa watoro na watu walioshindwa wakati walipoungana na Daudi.

Kati ya watu hawa mashuhuri wa Daudi, unaweza kuona ukweli huu tena ambao ulikuwa umedhihirishwa katika maisha ya watu kama Musa, Waamuzi wote, na hata Daudi mwenyewe. Ukweli huu ni kwamba Mungu hupenda kutenda mambo yasiyo ya kawaida kupitia watu wa kawaida. Zaburi kama hili la thelathini na nne na tukio lote kuhusu watu hawa mashuhuri wa Daudi yanadhihirisha yale yanayotajwa kama siri nne za kiroho. Siri hizo ni:

Si mimi, ila Mungu ndiye, naye yupo pamoja nami.
Mimi siwezi, lakini Mungu anaweza, naye yupo pamoja nami.
Mimi sitaki, lakini Mungu anataka, naye yupo pamoja nami.
Mimi sikutenda hivyo, lakini Mungu aliatenda kwa kuwa alikuwa pamoja nami.

Zaburi Ya Arobaini Na Sita

'Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake…Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu, patakatifu pa maskani zake Aliye juu. Mungu yu katikati yake hautatetemeshwa…Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu, Nitakuzwa katika mataifa, nitakuzwa katika nchi. Bwana wa majeshi yu pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.' (Zaburi 46:1-5, 10,11).

Kwa wana wake Kora, mwandishi wa zaburi ambaye aliandika zaburi hii, kuhusu milima kuanguka katika bahari, ulikuwa ni usemi wa kushangaza na usio na kifani. Kiini cha ujumbe huu wa ndugu Walawi ni kwamba wakati ulimwengu wetu kwa hakika unaposambaratika na kuvunjika, twahitaji kutulia kwa kitambo ili tufahamu kwamba Mungu ndiye–na yale anayotaka (10). Ulimwenguni kote, watu walitazama kwa mshangao wakati minara miwili jengo la biashara ya *World Trade Centre* huko Marekani yalipoporomoka. Huu ni mfano wa hivi karibuni kuhusu uharibifu usio na kifani. Huo ulikuwa ni mlima wetu ulioporomoka na kutumbukia baharini.

Twahitajika kutilia mkazo kweli ya ulimwengu huu, kuwa zipo dhamana za muda kidogo na pia za uzima wa milele. Misemo ya waandishi wa kale kwa dhana hii ya uzima wa milele na za muda kidogo zikiwa kando kwa kando, ni mto wenye kutiririka kupitia uharibifu huu wa kibinafsi, mali na ulimwengu huu wa muda tu, na kwamba mto hauwezi kuharibiwa. Mungu yupo katikati mwa mto huu, ambao hutiririka kupitia ulimwengu huu na kuleta furaha kuu katika mji wa uzima wa milele wa Mungu. Mtume mkongwe Yohana aliwaeleza watu wa Mungu hivi*, 'Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele'* (1 Yohana 2:17).

Ukweli kwamba mto huu hauwezi kusogwa unamaanisha kuwa unaweza kuiwakilisha dhamana za uzima wa milele ambazo hupitia ulimwenguni na mali hii ya muda tu. Wandishi hawa wa zaburi wanatueleza kwamba kakati ulimwengu wetu wa hakika, twahitajika kutulia kitambo ili kutilia mkazo kweli kwamba Mungu ndiye, na cho chote kile kinachohusika naye, ni cha milele!

Tunaelezwa katika Agano Jipya kwamba hatuwezi kumwendea Mungu wala hatuwezi kumpendeza isipokuwa tu, au hadi wakati tunapoamini kwamba Yupo. (Waebrania 11:6). Kulingana na zaburi hii, wakati ulimwengu wetu unapovunjika-vunjika, baada ya kuthibitisha kweli kwamba

Mungu yupo, pia twahitaji kutulia kitambo ili tufahamu mapenzi yake Mungu. Mapenzi yake Mungu ni kutukuka katika mataifa na ulimwengu kote. Zaburi ya arobaini na sita inatuambia kuwa wakati wa dhiki, twahitajika kutulia na kufahamu kwamba Mungu ana mapenzi kuhusu ulimwengu wetu–na maisha yetu binafsi.

Zaburi hii ina maneno mengi kuhusu faraja na mtazamo wa kiroho kwetu wakati ulimwengu wetu wa hakika au wa kibinafsi unaposambaratika. Maelezo yaliyomo katika tafsiri nyingine za Biblia hueleza kwamba waandishi hawa wa zaburi walikuwa wakituambia kwamba Mungu wetu 'amejitolea kwetu katika utajiri mkuu ili kutusaidia wakati tumesongwa kabisa.' Wakati walipotuambia tutulie na kufahamu kwamba Mungu ndiye, na mapenzi yake Mungu ni yapi, wao kwa hakika waliandika hivi: 'Tulia, acha kung'ang'ana, achilia kabisa, na ufahamu kwamba mimi ndimi, na kwamba mimi ndimi kila kitu ambacho Neno Langu lazungumzia. Pia, ufahamu kwamba mimi niko pamoja nawe wakati wa dhiki, na nina mapenzi kuhusu njia ile ambayo wahitajika kukumbana na hali iliyovurugika.'

Wakati watu wa Mungu wanapodhirika kwa kupoteza mali yao ya ulimwengu kupitia maafa, kama tetemeko la ardhi, mafuriko, janga la moto, au maafa yenye kuletwa na wanadamu kama vita; ingawa hakuna maafa mazuri, mara nyingi Mungu hutumia maafa haya ili kuwafunza watu wake tofauti kati ya hazina zilizopo mbinguni na hazina zilizopo ulimwenguni. Yesu alitufunza kuweka hazina zetu mbinguni kwa kuwa hazina za ulimwenguni huaribika na wevi huvunja na kuiba. (Mathayo 6:19-21).

Zaburi hii inatambulika kama unabii kwa kuwa inatumia lugha ya usemi na methali kuhusu kile manabii pamoja na mitume wanachotaja kama, 'Siku ya Bwana.' Wakati manabii wanapotabiri tukio, wao huonyeshana kana kwamba tayari limetukia. Hii inatajwa kama 'tendo kamilifu la unabii.' Wandishi wa zaburi hii wanaonyesha kana kwamba 'Siku Ya Bwana' tayari imefika, na wanatuongoza katika ziara ya kukadiria uharibifu, jinsi liwali au kiongozi wa nchi anavyopaa kwa ndege juu ya maeneo ya uharibifu na kukagua hasara'. Kwa hali hiyo, basi mistari ya kufungua na kufunga inarudiwa na kutupa changa moto kutulia na kufahamu kwamba Mungu ndiye, na mapenzi yake ni yapi (1, 10, 11). Maandiko yote ambayo yanatueleza kuhusu Siku ya Bwana, hutilia mkazo, 'jinsi twahitajika kuwa, huku tukifahamu kuwa vitu vyote vya dunia vitaharibiwa?' (1Pet. 3:10,11).

Wakati minara miwili ya jumba la biashara la *World Trade Centre* huko Marekani ilipolipuliwa, pamoja na maafa mabaya ya maisha ya watu walioangamia, ishara kuu za kidunia zenye kuwakilisha

dhamana za mamilioni ya watu ziliharibiwa kabisa. Mungu hana uhusiano na majambazi wenye vitisho na maafa, na hakuna jambo nzuri katika maafa ambayo hupata kutoka kwa watu waovu. Hata hivyo, wakati mwingine Mungu huyatumia maafa kama ishara ya kutuzindua kutoka usingizini na kuwa macho katika mfumo wa dhamana za kiroho na uzima wa milele. Hili ndilo shina lililopo katika ujumbe wa zaburi hii iliyoandikwa na wana wa Kora.

SURA YA NNE

KITABU CHA MITHALI

Wakati unapofanya biashara, kuna mambo mawili ambayo wanakufaidi–Fedha na Ujuzi. Wakati watu wenye haki wanapofanya biashara, watu wasio mcha Mungu hupata fedha ilhali watu wamchao hufaidika na ujuzi. Mungu alitupa kitabu hiki cha Mithali ili tusijifunze kila kitu maishani kwa njia ya ujuzi.

Kitabu cha Mithali kina matumizi mengi ya kimaisha kuliko vitabu vile vingine. Sulemani aliandika takribani Mithali elfu tatu (1 Wafalme 4:29-34). Yeye anashiriki nasi karibu Mithali elfu moja yenye uvuvio katika kitabu hiki. Alifahamika kama mtu mwenye hekima zaidi kuwahi kuishi. Katika kitabu hiki cha Mithali, yeye pamoja na watu wenye hekima kuu siku hizo wanatuonyesha jinsi ya kuishi maisha hasa katika nyanja za kimatendo.

Sulemani aliandika zaidi ya nyimbo elfu moja. Katika kitabu cha Mithali, tunakumbana na mithali chini ya elfu moja, na wimbo tu mmoja katika Biblia, yaani Wimbo ulio Bora. Sulemani hakuandika mithali yote iliyo katika kitabu cha Mithali. Yeye alikusanya pamoja baadhi ya misemo ya busara ambayo ilikuwa imeandikwa na watu wenye hekima, nao watu wengine wenye hekima walikusanya baadhi ya misemo yake Sulemani ambayo tunaipata katika kitabu hiki.

Sura za kwanza tisa zinakiri kwa dhati kusudi la kitabu hiki, ambalo ni kufundisha hekima. Mithali yake Sulemani inapatikana katika sura ya 10:1 hadi sura ya 22:16. Mithali za watu wengine wenye hekima zinapatikana katika sura ya 22:17-24-24:34, ilhali mithali za Sulemani ambayo wenye hekima wa Hezekia walikusanya ziko katika sura ya 25-29. Sura ya 30 ni maandishi ya Aguri, ilhali

sura ya 31 ni mithali zake mfalme Lemueli, ambayo alipokea kutoka kwa mama yake. Sura ya 1-10 zimeandikwa kwa vijana; nao sura ya 11-20 kwa wanaume wote; na hatimaye sura za 21-31 kwa viongozi wa watu.

Ingawaje Sulemani alifahamika kama mwenye hekima kuu kuliko ye yote kuwahi kuishi (1 Wafalme 4:31), kwa upande mwingine, yeye pia alikuwa mtu ambaye aliwahi kushindwa sana kuwahi kuishi. Jinsi tulivyotambua katika ukachuzi wetu wa vitabu vya historia, ufalme uliogawanyika pamoja na utekaji na uharibifu uliotokea huku Yerusalemu ni matokeo ya dhambi yake Sulemani, wala sio kwa sababu ya dhambi ya babake Daudi. Je, inawezekana mtu aliyewahi kushindwa namna hii kuwafundisha watu wa Mungu jinsi ya kuishi?

Kuna majibu kadhaa kwa swali hilo. Hekima iliyo katika mithali hii haitengemei kama mwandishi alitumia hekima hiyo katika maisha yake au la; bali inawakilisha hekima yenye uvuvio ya Mungu. Pia, Mithali hii, Zaburi 127, na kitabu cha Mhubiri, ziliandikwa na Sulemani ili kuwafunza vijana kwamba wasitende yale aliyoyatenda. Yeye alijifunza mengi kutokana na makosa yake, kwa hivyo alitaka kuwapa hekima hii yake aliyoipata kupitia kazi ngumu, hasa vijana.

Sawa na vile Sulemani anavyotaja kusudi la Mithali hii, aandika hivi: *'Nimekufundisha katika njia ya hekima; Nimekuongoza katika mapito ya unyofu…Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, watashiba mashauri yao wenyewe…Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima; Na kumjua Mtakatifu ni ufahamu'* (4:11; 1:31; 9:10).

Kwa njia nyingine, lengo kuu la Sulemani ni ufupisho wa ujuzi aliokuwa nao katika maisha. Yeye alifahamu kwamba alikuwa ameshindwa lakini alitaka tufahamu kwamba sisi twajifunza hekima kutokana na kushindwa pamoja na matokeo yake. Njia moja iliyo bora kujifunza kutokana na dhambi na makosa ya kushindwa kwetu ni jinsi ambavyo tunakumbana na matokeo yale. Tunapokumbana na dhiki na vurugu ya njia tulizozichagua wenyewe, huwa tunalipia gharama kuu ili kupata hekima. Nasi hudhibitisha kwa ujuzi kwamba 'maisha ya matendo yanaokumbalika ndio hekima kuu ilipo.'

Wakati Mungu anasema kwamba jambo fulani ni sawa, Yeye hutuambia hivyo kwa kuwa anatupenda. Yeye hututakia lililo jema kwa kuwa anafahamu matokeo ya matendo mema. Wakati Mungu atangazapo kwamba kitu fulani ni kibaya, yeye hufanya husema hivyo kuwa anafahamu matokeo ya mambo mabaya.

Maonyo Kumhusu Mwanamke Mwenye Kudondoza Asali

Mithali 5:15-19 kinaelezewa vijana kuwaonya kuhusu majaribu ya mwanamke mwenye kudondoza asali. Mistari hii hufundisha kinga iliyo bora dhidi zinaa-kinga yenye nguvu ambayo ni ndoa. Vijana wanahitajika kutoshelezwa nao upendo wa wake zao nyakati zote. Sulemani anawaandikia vijana wa kiume hivi: *'Chemichemi yako ibarikiwe; Nawe umfurahie mke wa ujana wako'* (18), ili kwamba wakati wanapokumbana na ulimwengu, hawatashawishiwa na urembo wa mwanamke mwenye tamaa. Wao hawatamfuata kwa kuwa tayari wametoshelezwa hamu ya ngono na wake zao. Maonyo yake Sulemani kwa mtu ambaye huangukia majaribu ya zinaa ndio haya: *'Naye atashikiwa kwa kamba za dhambi zake. Atakufa huyo kwa kukosa maonyo, Naye atapotea kwa wingi wa ujinga wake'* (22b, 23).

Nidhamu Ya Kibinafsi

Ili kufundisha juu ya umuhimu wa nidhamu ya kibinafsi, Sulemani alisema: '*Ewe mvivu, mwendee chungu, zitafakari njia zake ukapate hekima. Kwa maana yeye hana akida, Wala msimamizi, wala mkuu,'* (6:6-7). Wakati sisi tungali wachanga, wazazi wetu pamoja na walimu wetu hutuzunguka, ili kutuonyesha yale yanayotarajiwa kutoka kwetu na kutuajibisha. Hata hivyo, tunapokua na kukomaa, huwa tanarajiwa kujisimamia wenyewe na kuwa na nidhamu ya kibinafsi. Kulingana na Sulemani, twaweza kujifunza nidhamu ya kibinafsi kutoka kwake chungu, ambaye bila ya usimamizi, huyaandaa malisho yake kwa wakati wa hari na ule wa mavuno kwa mwaka mzima.

Kutoa Na Kupokea

Kuna mafunzo katika kitabu hiki cha Mithali yanayolingana na mafundisho ya Yesu (11:24-25). Yanasema hivi: *'Kuna atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; Kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji. Nafsi ya mtu mkarimu itawandishwa; Anyweshaye atanyweshwa mwenyewe.'* Mithali hii hufundisha kwamba nafsi zetu hulishwa wakati sisi tu wakarimu, lhali hukaa njaa wakati tunapokosa kuwa wakarimu. Kama tukishikilia kile tulicho nacho, twaweza kukipoteza chote tulicho nacho, lakini ikiwa tutakipeana kwa ukarimu, basi tunafanyika kuwa matajiri. Yesu alitoa kanuni hii wakati alipofundisha kwamba ni lazima tusalimishe maisha yetu ili tupokee uzima wa milele (Mathayo 16:24-27; Matendo 20:35). Kulingana na Yesu, kwa hakika kupata maisha yako ni lazima uyapoteze, uyamwage nje, au uyafanye kuwa dhabihu kwa Mungu na watu wengine.

Unaweza kutarajia kuvuna hekima katika kitabu cha Mithali kwa kuwa ni cha misemo yenye hekima. Kumbuka kwamba kusudi lake Sulemani kukusanya misemo hii ni kwamba wenye hekima wafanyike viongozi wenye hekima, nao wapumbavu wafanyike wenye hekima, na watu wapate kufahamu jinsi ya kuishi vyema.

Kwa sababu kuna siku thelathini au thelathini na moja katika mwezi mmoja, vijana wahitajika kukitumia hiki kitabu kama kalenda kwa kusoma sura inayolingana na siku ile ya mwezi. Nakusihi utengeneze kijitabu chenye ramani yenye michoro zaidi ya kumi na miwili toka juu hadi chini. Kutoka upande wa kushoto moja hadi mwengine, juu ya mistari hiyo ya kugawanya, andika maneno hivi, 'nidhamu ya kibinafsi au wanawake au nidhamu ya watoto wachanga,' na kadhalika. Unaposoma kitabu hiki, linganisha mistari uisomayo pamoja na maneno yale uliyoandika kwenye daftari ile. Utakapomaliza, utakuwa na jarida la taratibu ya mafunzo makuu yaliyo katika kitabu hiki cha hekima.

Maneno kama moyo, roho, na nafsi yametajwa mara sabini katika kitabu hiki. Hili linaonyesha kwamba Mungu huzungumzia moyo, roho, na nafsi zetu wakati anahitaji kutufundisha jinsi ya kuishi vyema. Mithali yenye maelezo ambayo huwavutia wengi wanaosoma kitabu hiki, ni: *'Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako'* (3:5-6).

SURA YA TANO

KITABU CHA MHUBIRI

Kitabu cha mhubiri huzungumzia mioyo ya watu wake Mungu wakati wanapotafuta majibu kwa mambo yenye utata katika maisha. Neno 'Mhubiri' linamaanisha kuhubiri, na kitabu hiki ni ujumbe uliohubiriwa naye Sulemani kwa vijana wakati wa machweo ya maisha yake. Hali au namna ya mahubiri haya ni kwamba hata ingawa ujuzi ni mwalimu mwenye ushawishi mkuu, pia siye mwalimu wa pekee. Sio lazima tujifunze kila kitu kwa ujuzi. Mhubiri akihimiza kizazi kichanga kijifunze kutokana na ujuzi wake. Ujumbe huu ni nakala yenye uvuvio kuhusu jinsi mtu mmoja alivyokuwa na sifa ya kuwa mwenye hekima kuliko mwanadamu ye yote kuwahi kuishi, aliyetafuta kwa makini na hekima yake yote kufahamu maana na kusudi la maisha, 'Neno La Mwisho La Hekima.' Mungu

ameutumia huu ujumbe kuizungumzia mioyo ya watu wake wakati wanapotafuta, kupeleleza, kuuliza, kuhoji, kutazama-tazama na hata wakati wanapokuwa kwenye mashaka.

Uchunguzi Mfupi Wa Mahubiri Haya.

Kitabu cha Mhubiri ndicho kitabu cha pili cha Sulemani kuhusu mashairi. Sulemani alikiandika kitabu hiki kwa vijana waliokuwa Israeli wakati yeye alipokuwa kikongwe. Jinsi tulivyojifunza katika Zaburi 127, wakati Sulemani alipokagua maisha yake kwa upeo wa juu katika ukongwe wake, pamoja na hekima aliyojifunza miaka mingi, yeye alikiri kwamba alifanya kazi kwa jitihada kuu, alihusika sana na kufanya ujenzi wa mambo mengi kwa ubatili. Maneno haya ni ufafanuzi mkuu kutoka Zaburi 127. Alilitoa ujumbe huu kwa kuwa alikuwa na tumaini kuu kwa vijana waliomsikiza kwamba wao watajifunza kutokana na ujuzi wake wenye kushusha moyo.

Hoja Tatu Kuhusu Maana

Katika kitabu cha Mhubiri, Sulemani aliwaambia vijana wa Israeli kwamba yeye alijaribu kutafuta kusudi na maana ya maisha katika maeneo matatu na kwamba mwisho wa kila hoja yake, yeye alikumbana na utupu wenye ubatili. Katika zaburi yake fupi, ambapo alikiri kushindwa, tulimsikia akisema, *'Bwana asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure. Bwana asipoulinda mji, yeye aulindaye akesha bure. Kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema, Na kukawia kwenda kulala, Na kula chakula cha taabu'* (Zaburi 127). Tutalipata neno hilo ambalo limetumika sana katika ujumbe huu wake Sulemani kuhusu kusudi na maana kuu ya maisha.

Utajiri

Sulemani alihubiri kwamba yeye alitafuta maana na kusudi ya maisha kwa njia ya kukusanya utajiri, naye akafanyika kuwa tajiri mkuu kuwahi kuishi. Hata hivyo, wakati alipoutazama huo utajiri kwa upeo wa maisha yake yenye kikomo, alisema, *'Nami nikaichukia kazi yangu yote niliyojishughulisha nayo chini ya jua; maana sina budi kumwachia yeye atakayenifuata'* (2:18).

Sulemani alikutana na mpumbavu sokoni na kutambua kwamba mtu yule ambaye angerithi utajiri wake, anaweza kuwa kama yule mpumbavu. Ukweli usio kubalika wa jambo hilo kutokea ulimfanya Sulemani kupiga chapa 'ubatili' kote katika ufanisi wa utajiri wake.

Hekima

Wakati Sulemani alipotambua kwamba utajiri haukuwa kusudi au maana ya maisha, alisalimisha maisha yake kutafuta hekima. Alifanyika kuwa mwenye hekima zaidi kuliko mwanadamu ye yote kuwahi kuishi, lakini hakupata kusudi hapo. Yeye aliona kuwa ubatili utajiri wake kwa sababu hangelichukua utajiri huo pamoja naye kwenye kaburi. Naye hakukawia kwa muda mrefu kabla ya kupiga chapa utafutaji wake wa kusudi na maana ya maisha katika hekima kuwa ubatili mtupu. Hii ni kwa sababu hangeweza kufasiri hekima ifanyike kuwa furaha: *'Yaani, Katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni; Naye aongezaye maarifa huongeza masikitiko'* (1:18).

Sanamu ya mwenye kufikiri sio picha ya mtu mwenye furaha. Ujinga ni heri na kutosheka jinsi fahali ni kutosheka ambako msingi wake ni ujinga. Kwa kuwa utafutaji kwa makini wa maarifa hauongezi furaha, Sulemani alipiga chapa kutafuta huku kwake maana na kusudi ya maisha katika hekima kuwa ni: UBATILI MTUPU.

Anasa

Kutafuta kulikofuata kwake Sulemani maana na kusudi kulimwongoza kukitafuta kicheko, starehe, na mzaha. Yeye alihusika katika anasa ambazo ulimwengu ungeweza kumpatia: *'Wala sikuyanyima macho yangu cho chote yalichokitamani; wala sikuuzuia moyo wangu katika furaha yo yote'* (2:10a). Hakuna mtu mwingine aliyewahi kuhusika katika anasa kama Sulemani alivyofanya. Lakini, baada ya anasa zake zenye zinaa za kila namna, Sulemani alibaki akiwa na hoja au maswali yake matatu: Wema wake ni nini? Kazi yake ni nini? Je! Nimetimiza nini? Sulemani aligundua kwamba ndani ya moyo wake, kulikuwepo na kusudi katika maisha yake na kusudi hilo halikuwa katika anasa usiku kucha.

Uamuzi

Kumalizia mahubiri yake, Sulemani alifikia uamuzi kwa kuwaambia vijana waliokuwa wakimsikiliza kwamba katika maisha yake, alijifunza kweli moja kuu: *'Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasavyo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya'* (12:13-14). Tafsiri ya Kiebrania iliyotumika hapa humaanisha kwamba kumcha Mungu na kuzishika amri Zake humfanya mtu kuwa mkamilifu. Kumcha Mungu ndio mwanzo wa hekima kwa kuwa

humfanya mwanadamu kufanyika jinsi atakikanavyo kuwa. Hili ndilo kusudi ambalo Sulemani alitafuta maishani mwake yote.

Hekima ya Sulemani ambayo inawasilishwa katika sababu hii kwa hakika ni yenye kujumuishwa kabisa kwa kuwa alikuwa wakati wote katika mahubiri yake akijadili kwamba maisha yake yamejaa ukosefu wa haki. Watu walirithi utajiri ambao hawakuufanyia kazi, wenye kusetwa hawakuipata faraja, na wale wenye utajiri mkuu mara kwa mara hawakutosheka. Kutokuwa haki, kutokulingana, na unyanyasaji dhidi ya maskini na wasiojiweza kutokana na watu waovu bila kujali, na maovu mengine mengi, yalimfanya Sulemani kukubali kwamba kulikuwepo na uamuzi wenye kujumuishwa kabisa.

Lulu Zenye Uvuvio Na Za Kweli Katika Mhubiri

Unapozidi kusoma kitabu cha Mhubiri, utatambua kwamba kuna njia mbili kuhusu kweli. Wakati mwingi, Sulemani aonekana akichukua wajibu wa mtu mwenye shaka, kuhoji na mwenye mashaka asiye na ufunuo kutoka kwa Mungu. Naye anajadiliana sawa na mtu asiye wa kiroho, mtu wa ulimwengu kabisa. Wakati mwingine, yeye hufikiria na kuzungumza kama mtu wa kiroho na mwenye ufunuo kutoka kwa Mungu. Ingawa Sulemani alieleza mashaka mengi katika mseto wa kwanza wa mawazo, kweli ambazo zinaelezwa kama mtu yule wa pili ni zenye ufunuo na ukweli mkuu na hutusaidia kuongeza ufahamu wetu kuhusu kusudi na maana ya maisha.

Kifungu katika sura ya tatu kinasema hivi, *'Kwa kila jambo kuna majira yake, Na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu. Wakati wa kuzaliwa, na wakati wa kufa; Wakati wa kupanda, na wakati wa kung'oa yaliyopandwa'* (3:1-2). Kifungu hiki kinafanana na kile kilio katika Zaburi ya kwanza ambayo inatueleza kwamba mtu aliyebarikiwa huzaa *'Matunda yake kwa wakati wake'* (Zaburi 1:3b). Kazi ya Mungu kwa maisha yake hufanyika wakati Wake mwenyewe.

Sulemani pia alitupa nuru yenye kuvutia katika ndoa wakati alipoandika*: 'Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingine wa kumwinua! Tena wawili wakilala pamoja, hapo watapata moto; lakini mmoja aliye peke yake tu awezaje, kuona moto? Hata ikiwa mtu aweza kumshinda yule aliye peke yake, wawili watampiga; wala kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi'* (4:9-12).

Wakati Mungu aliufanya mfumo wa uhusiano wa ndoa, mapenzi yake yalikuwa mwanamume pamoja na mkewe wawe kitu kimoja katika nia, mwili, na roho. Mpango wake ulikuwa na bado ni kwamba utu wa ndani katika kiroho chetu na nia zetu udhihirishwe katika mwili kwa hali ya ngono. Yawezekana haya ndiyo yaliyokuwa mawazo ya Sulemani aliposema kwamba kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi. Ndoa kwa upeo wa huu, ngono ni aina ya mawasiliano ya hali ya juu sana. Ikiwa uhusiano wa kimwili katika ndoa siyo dhihirisho ya yale yaliyomo ndani katika nia na roho, basi ngono katika ndoa ile ni sawa na uhusiano wa wanyama katika mawasiliano.

Katika sura ya tisa, Sulemani anaelezea mji ambao ulikombolewa kupitia mtu mwenye hekima: '*Palikuwa na mji mdogo, na watu ndani yake walikuwa wachache; akaja mfalme mkuu juu yake, akauhusuru, akajenga ngome kubwa ili kuupiga. Basi, kulionekana huko mtu maskini mwenye hekima, naye kwa hekima yake akauokoa mji ule, lakini hata hivyo hapakuwa na mtu ye yote aliyekumbuka yule mtu maskini'* (14,15). Sulemani alielezea juu ya kusahaulika kwa yule maskini kama jambo lisilokuwa la haki. Hata ingawa juhudi zake huyu mtu mwenye hekima hazikupewa thawabu, yeye aliufikia ukweli kuwa, *'maneno ya wenye hekima yanenwayo taratibu husikiwa, Zaidi ya mlio wake atawalaye katikati ya wapumbavu'* (17). Kwake yeye, kutendwa kwa kazi kulikuwa muhimu sana kuliko kupokea thawabu kwa kuitimiza kazi.

Sulemani akimalizia ujumbe wake, aliwashauri vijana wachanga *'mkumbuke Muumbaji wako siku za ujana wako,'* (12:1). Yeye alifahamu kwamba wakati wa ujana ulikuwa wa baraka na uzalishaji, lakini pia alifahamu kwamba uzee huingia upesi. *'Mkumbuke Yeye,'* Sulemani aliwahimiza, *'kabla haijakatika kamba ya fedha; au kuvunjwa bakuli ya dhahabu…Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa'* (6, 7). Wale wangali ujanani watafanya vyema kama watamkumbuka Mungu na kuishi maisha yao vyema kwa kuwa mwishowe watakumbana naye. Na baada ya yote, Sulemani alikusudia, kwamba maana ya maisha ilipatikana katika tangazo lake la mwisho*: 'Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu'* (13).

SURA YA SITA

KITABU CHA WIMBO ULIO BORA

Wimbo Ulio Bora ndicho kitabu cha mwisho katika vitabu vya mashairi. Twaelezwa kwamba Sulemani aliandika takribani nyimbo elfu moja na tano, lakini huu ndio wimbo ambao ulihifadhiwa kwetu kwa njia ya maandiko. Wimbo huu wa mapenzi ni nakili ya mahaba na maongezi ya huba kati ya wapenzi wawili. Vijana wadogo wa Kiebrania hawakuruhusiwa kukisoma kitabu hiki hadi walipotimia umri wa miaka thelathini.

Labda unashangazwa ni kwa sababu gani kitabu hiki kipo miongoni mwa vitabu vilivyo katika maandiko. Yapo majibu kadhaa kwa swali hilo. Kitabu hiki kinatufundisha utakatifu wa kitanda cha ndoa. Katika kitabu cha Mwanzo, tulimsikia Mungu akisema kwamba *'Siyo vyema mwanadamu kuwa peke yake'.* Kwa hivyo Mungu akamuumba mwanamke ili kumkamilisha Adamu. Wakati Mungu alipomuumba mume na mke, aliwaleta pamoja katika uhusiano wa ngono. Kulingana na nakala ya uumbaji, baada ya Mungu kuumba, alitangaza kile alichoumba kuwa chema. Wakati Mungu alipoiumba ngono, alitangaza kwamba 'ngono ilikuwa ni nzuri sana.'

Ikiwa hakungekuwa na maana kuu katika wimbo huu wa mahaba, ujumbe wa utakatifu katika ngono ni muhimu tu katika kitabu chenye kuvutia ili kuwa sehemu ya maktaba takatifu tunayoita 'Biblia.' Ni muhimu sana kwa wazazi kuwafunza watoto wao kwamba ngono ni njema sana. Ni changa moto kwetu kuwahimiza watoto wetu kuhifadhi ngono hadi katika ndoa bila kuwaonyesha kwamba ngono dhambi. Ikiwa tutawashawishi watoto wetu kwamba ngono dhambi, basi twaweza kuwajeruhi hisia zao kuhusu ngono katika ndoa. Wao wanaweza kuingia katika ndoa wakiwa na dhana ambayo ni mbovu kuhusu ngono na hii inaweza kuwazuia furaha ya ngono katika ndoa.

Wimbo huu wa mahaba unatufundisha kwamba Mungu hubariki, hukubalisha na kuvuvia kitanda cha ndoa na 'furaha kuu ya ndoa.' Unapozidi kusoma huu wimbo wa mahaba, utaona kusudi lake Mungu likithibitishwa kwa furaha inayodhihirika katika uhusiano wa karibu wa upendo wa ngono kati ya mume na mke kwa hali ya ndoa.

Wakongwe wa imani wametambua kwamba kuna maana nyingine kuu katika Wimbo Ulio Bora. Wao huona maana kuu yenye kulingana sambaba na uhusiano wa wapenzi wawili sawa na uhusiano baina yetu na Mungu pamoja na Kristo, ambao huelezwa kama uhusiano wa ndoa. Wao huamini kwamba Wimbo Ulio Bora uliwekwa katika maandiko kama mfano wa upendo wake Yehova Mungu kwake Israeli. Unaposoma Agano Jipya, utagundua kwamba methali au mfano huu wa mahaba au upendo pia unatumika kwake Kristo na Kanisa lake. Kristo ndiye bwana harusi nalo kanisa ndio bibi harusi (Mathayo 25:1-13; Ufunuo 21:2,17).

Ushirika Na Ibada Iliyo Katika Wimbo Ulio Bora

Mfano wa mwisho ambao uko katika wimbo huu wa mahaba unahusu uhusiano wetu wa kibinafsi naye Kristo anayeishi. Katika Agano la Kale, Israeli waliamrishwa kumpenda Mungu kwa mioyo yao yote. Yesu alithibitisha funzo hili wakati alipoulizwa kuitaja sheria iliyo kuu kuliko nyingine kati ya sheria (Mathayo 22:35-40). Uhusiano wa upendo wetu wa kibinafsi kwake Mungu pamoja na Kristo unaelezwa kwa njia ya kuvutia mno katika hadithi hii ya mafumbo kuhusu hawa wapenzi wawili. Tafsiri hii na matumizi ya Wimbo Ulio Bora hukifanya kitabu hiki kuwa cha ibada miongoni mwa vitabu vingine katika Biblia–na ambacho hutufundisha zaidi kuhusu uhusiano wa karibu naye Kristo aliyefufuka na anayeishi.

Uhusiano Unaolingana Na Ibada Katika Wimbo Ulio Bora

Bibi harusi katika Wimbo Ulio Bora kwanza alimchukua Bwana harusi katika chumba chake (1:4), na baadaye katika meza ya sherehe (2:4). Hii inamaanisha kwamba uhusiano wetu naye Kristo wahitajika kwanza kuwa wa karibu. Yesu aliyazungumzia haya kwa kirefu katika mahubiri yake mlimani. Yeye aliwashutumu wale ambao waliyaelekeza maombi yao kwenye umati na kuyafanya matendo yao mema kuonekana kwa watu wengine kwa kuwa maombi yao na kutoa kwao yalifanyika kwa faida ya wanadamu, nasi kwa faida yake Mungu (Mathayo 6:5-7).

Himizo lake Yesu lilikuwa kwamba maombi yetu yahitajika kufanywa kwake Mungu na kutoa kwetu kufanyike kwa Mungu bila mtu mwingine kufahamu. *Martin Luther* aliandika hivi: *'Mtakatifu Yesu, mpole mwana, jifanyie mwenyewe kitanda, chororo, kisicho na uchafu ndani mwa moyo wangu ili kiwe ni chumba chenye kimya kilichohifadhiwa kwa ajili yako.'* Je, moyo wako unao kimya na umehifadhiwa kwa ajili Yake peke Yake?

Hakuna wakati mawasiliano kati ya wapenzi wawili katika Wimbo Ulio Bora, yalivunjika kwa mapenzi yake Bwana Harusi. Picha hii inafafana na ushirika wetu kwake Kristo. Ushirika wetu kwake unaweza kuwa ushirika usio na kikomo, lakini kama ukivunjwa, huwa ni sisi wenyewe tumeuvunja, wala si Kristo. Uhusiano wetu uliovunjika sio kuwa Kristo ametuhadaa, bali kwa kuwa sisi sio waaminifu kwake.

Wakati Bwana harusi anapokitembelea chumba chake bibi harusi, yeye hufungiwa nje, huku bibi harusi akiwa na shughuli za kibinafsi, kama kujipodoa na kuweka marashi yake na mambo mengi ya urembo. Mwishowe anapoufungua mlango, yeye humpata ametoweka (5:1-6). Wakati mwingi sisi husongwa na upako na karama zake Roho kiasi kuwa tunasahau ushirika wetu pamoja na mwenye kutupa karama hizo za kiroho. Katika shughuli zetu na udhihirisho wa karama za Roho Mtakatifu, sisi humwacha Bwana harusi, ambaye angelipenda kuwa na uhusiano wa karibu nasi, akiwa amesimama nje ya mlangoni.

Bibi harusi katika Wimbo Ulio Bora hufahamu kazi yake Bwana harusi*: 'Twende mapema hata mashamba ya mizabibu, tuone kama mzabibu umechanua, Na maua yake yamefunuka; Kama mikomamanga imetoa maua'* (7:12). Kulingana na yale Yesu aliyomwambia Petro katika Injili ya Yohana, tunaweza kuudhihirisha upendo wetu Kwake kwa kuonyesha kuhusika kwetu na kundi lake, kwa kuwachunga kondoo, na kwa kuwapenda kondoo ambao Yeye awapenda kwa upendo mkuu (Yohana 21:15-17).

Matumizi makuu ya shairi hili ya kuvutia sana ni yapi? Wimbo Ulio Bora unazungumza kwa lugha ya moyo kuhusu hisia muhimu: Upendo. Unaelezea uhusiano muhimu sana ambao tunaweza kuwa nao–uhusiano wetu na Kristo–na kwa njia ya mfano tukipewa maelezo kuhusu upendo wake kwetu sisi, na kuitikia kwetu kwa Upendo Wake.

Ili kuelewa dhamana hii ya kipekee ya upendo, ni lazima tuanze na upendo wake Mungu. Kuna mahali mbili katika Agano Jipya ambapo tunapata upendo wake Mungu ukichunguzwa na kuonyeshwa. Katika sura ile ya upendo ya mtume Paulo na katika sura ile nyingine ya upendo katika Injili ya mtume Yohana, upendo wake Mungu hupitishwa katika mwanga wenye uvuvio katika mawazo yao na kutokea upande mwingine kama kivufurusi cha wema (1 Wakorintho 13; 1 Yohana 4:7-21). Yohana na Paulo wanatueleza kuhusu upendo wake Mungu kwamba: hauwezi kubadilishwa,

hauelezeki, hauharibiwi na cho chote, hauna masharti, hauna pingamizi, ni wa kiroho, ni wa milele na sio wa kawaida.

Wakati tunapopendana tukiwa na dhamana hizi za upendo, tunakuwa na uwezo wakumpenda mwenzi wetu, watoto wetu, na wazazi wetu, na wale ambao wapo katika maisha yetu ambao labda ni vigumu kuwapenda. Wimbo Ulio Bora unatufundisha kwamba upendo tulio nao kwake Kristo ni wa kibinafsi, wa karibu, wenye kuhusisha, usio wa kujipenda, wenye kukubalika, wakutosheleza, wenye kujenga, usio wakutisha, na ambao hauzimiki.